Nipashe
Alhamisi Aprili 22, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580558
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**TANZANIA** yashinda kesi ya mabilioni nchini Marekani

UKURASA 3



**WAFANYABIASHARA** wakubali kushusha bei mafuta ya kula

UKURASA 3

ama — AFYA NA MAZINGIRA



MAZINGIRA YENYE KITENDAWILI MABINTI KUANZISHA FAMILIA KATIKA UTANDAWAZI



Migogoro ya familia yaziita kwa kasi VVU na madhara kwa mabinti zao

**Mkurugenzi Kinga: Ukihisi ujauzito, mara moja anza mchakato huu hapa**

• Dk. Maro, ataja vigingi utakavyovikuta



UKURASA 11

# Kikwete, Kinana waibua mjadala

UK. 2



## Kishindo cha Samia kutikisa Bunge leo

UKURASA 2

**RIPOTI MAALUM**

## Mlipuko wa aina yake waja kidato cha kwanza 2022

UK. 4

**MICHEZO** NCHIMBI AFUNGUKA KUHUSU YANGA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa China hapa nchini, Janson Huang (wa pili kushoto), aliyeambatana na viongozi wenzake, Ikulu Chamwino jijini Dodoma jana. Habari Uk. 5. **PICHA: IKULU**

# Akaunti za THRDC zafunguliwa rasmi

**Na Salome Kitomari**

AKAUNTI za Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) zilizokuwa zimefungwa kwa takribani miezi minane, zimefunguliwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa umma na Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao huo, Vicky Ntetema, alisema akaunti hizo zilifungwa tangu Agosti mwaka 2020.

Alisema kufungwa kwa akaunti hizo kulisababisha mtandao kushindwa kutekeleza sehemu kubwa ya majukumu yake kwenye miradi ya utetezi wa haki za binadamu kama ilivyokuwa kwenye mipango ya mwaka 2020.

"Kufunguliwa kwa akaunti hizo kumetokana na maelekezo ya mamlaka za serikali zilizoagiza kufungwa, ili uchunguzi wa tuhuma ufanyike na kisha kutoa maelekezo kuwa zifunguliwe," alisema.

Kwa mujibu wa Ntetema, mtandao utaendelea kufanya kazi bila hofu, kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu zote zilizowekwa na mamlaka zote ikiwamo ofisi ya uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuendelea kudumisha na kuboresha ushirikiano katika kazi za utetezi wa haki za binadamu.

"Mtandao unaahidi kuendelea kufanya kazi kwa ukaribu na kwa kushirikiana na wadau na viongozi mbalimbali, mamlaka za serikali, asasi za kiraia, mahakama, Tume ya Haki za Binadamu.

"Wadau wa maendeleo, vyombo vya habari, wanasheria, taasisi za kitaaluma, Ofisi ya Msajili wa Asasi za Kijamii na wanachama wake, ili kuhakikisha utetezi wa haki za binadamu unafanyika kwa ufanisi na weledi mkubwa," alisema.

Ntetema alisema bodi inamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake unaojali na kuzingatia haki za binadamu na utawala bora.

Katika taarifa yake hiyo, mtandao huo pia unawashukuru watu wote, wahisani, taasisi mbalimbali na wanachama wa mtandao walioshiriki kwa namna mbalimbali kuhakikisha mtandao unaendelea kutekeleza majukumu yake na kuhakikisha vikwazo vinatatuliwa.

Nipashe ilipodadisi kuhusu usalama wa fedha zilizokuzokuwamo kwenye akaunti hizo, mtandao huo ulibainisha kuwa fedha zake zote zipo kwenye akaunti.

# JK, Kinana waibua mjadala bungeni

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

HATUA ya watumiaji wa mitandao ya kijamii kutuma picha ya Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, Katibu Mkuu wa zamani wa CCM, Abdulrahman Kinana, kuwasema vibaya imezua jambo bungeni.

Mbunge wa Makambako (CCM), Deo Sanga, akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2020/21, alitaka tabia ya kuwasema vibaya viongozi hao isitishwe kwa kuwa ni hatari kwa usalama wa nchi.

Kutokana na hatua hiyo, Sanga aliomba serikali ikomeshe haraka huku akiwataja viongozi wengine wanaoandamwa na kusemwa vibaya kwenye mitandao ya kijamii kuwa ni Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye na Spika wa Bunge, Job Ndugai. "Tangu Rais Jon Magufuli alipofariki dunia, vitu vinavyowekwa kwenye mitandao ya kijamii ni hatari kwa usalama wa nchi yetu. Picha ya Kinana, Spika, Nape na hata Rais Mstaafu Jakaya Kikwete zinawekwa sana na kuzungumzwa mambo mazito ambayo yasipodhibitiwa kunaweza kuhatarisha usalama wa nchi.

"Nani asiyefahamu mchango wa Nape na Kinana mwaka 2013/14 wa kukipigania chama walipozunguka nchi nzima kutafuta kura za CCM hadi Nape akaumia bega. Leo wanazushiwa mambo mabaya? Haikubaliki," alisema.

"Rais Mstaafu Kikwete wamwache apumzike, amefanya kazi yake vizuri, Kinana akapumzike. Na wewe Ndugai wameanza kukuweka katika mitandao, wakuache ufanye kazi yako vizuri. Suala la Bandari ya Bagamoyo Spika amefanya kosa gani? Yeye amesema suala hilo lijadiliwe".

Kutokana na hoja ya Sanga, Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kirumbe Ng'enda, alisimama na kuomba mwongozo wa Spika.

"... Mchangiaji ameleta hoja kutoka mitandao ya kijamii, kama inaruhusiwa kuleta reference (rejea) za mitandaoni hapa bungeni. Kwa sababu hata mimi niliwahi kuuawa (kuzushiwa) mara mbili mitandaoni, pia nilizushiwa nimeparalyze (kiharusi)".

Hata hivyo, Spika Ndugai alijibu: "Kanuni zinaniruhusu kutoa ufafanuzi wa mwongozo hapo hapo au siku nyingine. Nami nimechagua kutolea ufafanuzi siku nyingine."

# Kishindo cha Samia kutikisa bungeni leo

**Na Waandishi Wetu,**
DODOMA

MACHO na masikio yanatarajiwa kuelekezwa bungeni jijini Dodoma leo, wakati Rais Samia Suluhu Hassan atakapolihutubia Bunge.

Kutokana na ujio huo wa Rais Samia bungeni, Spika wa Bunge, Job Ndugai, amewataka mawaziri na wabunge wote walioko nje ya Jiji la Dodoma kuhakikisha wanakuwapo bungeni leo.

Kwa mujibu wa Spika Ndugai, Rais Samia anatarajiwa kulihutubia Bunge majira ya saa 10 jioni, akibainisha kuwa pamoja na mambo mengine, hotuba hiyo itajikita katika kuelezea mwelekeo wa serikali yake.

Spika Ndugai jana aliwataka mawaziri, manaibu wao na wabunge kuhakikisha wanakuwapo bungeni wakati Rais Samia akitoa hotuba yake hiyo.

Spika Ndugai alisema hotuba ya Rais Samia ni muhimu kwa wabunge wote na Watanzania, hivyo ni lazima kila waziri na mbunge kuwamo ndani ya mhimili huo leo.

Kwenye taarifa yake Spika Ndugai alisema: Ninaomba nisisitize kwamba kesho (leo) kila mtu lazima awamo bungeni. Ninaomba wabunge muwapigie simu wenzenu ambao hawapo Dodoma. Hata mawaziri waliopo nje ya Dodoma waache shughuli zao na warejee haraka bungeni kuja kumsikiliza Rais Samia."

Spika Ndugai alisema kutachukuliwa kumbukumbu kwa wabunge wataohudhuria tukio hilo, kwamba ni lazima kila mbunge awapo kwa sababu kuna masuala yatamhusu moja kwa moja.

Ni mara ya kwanza kwa Rais Samia kulihutubia Bunge tangu alipoapishwa kuwa Rais Machi 19 mwaka huu baada ya kifo cha Rais wa tano, Dk. John Magufuli kilichotokea Machi 17 mwaka huu.

**BAWACHA WALIA**

Katika hatua nyingine, Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) limemwomba Rais Samia, wakati wa kulihutubia Bunge leo kutoa tamko kuhusu wabunge 19 waliotokana na chama hicho walioapishwa na Spika Ndugai, likidai kuapishwa kwao ni kinyume cha katiba ya nchi.

Mweka Hazina wa BAWACHA Taifa, Catherine Ruge, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipotoa tamko la baraza hilo kwa waandishi wa habari.

Alisema wabunge hao wako bungeni lakini waliingia kutokana na kukiukwa kwa katiba ya nchi kwa kuwa tayari walishavuliwa uanachama na Kamati Kuu ya CHADEMA tangu Novemba mwaka jana.

"Tunamwomba Rais Mama Samia kulitolea tamko suala hili kwani wabunge hawa 19, wameingia pale kwa kuvunja katiba ya nchi na Rais ameapa kulinda katiba ya nchi, hivyo tunamwomba kulitolea tamko suala hili," alisema.

**●Imeandikwa na Gwamaka Alipipi na Paul Mabeja**

HABARI KITAIFA

# Wafanyabiashara wakubali kushusha bei mafuta ya kula

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SAA 24 alizotoa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, kuwataka wafanyabiashara waliopandisha maradufu bei ya mafuta ya chakula, sukari na nyama, kushusha bei, zimejibu baada ya wafanyabiashara hao kutii agizo hilo.

Wafanyabiashara wa maduka ya jumla na rejareja walipandisha bei ya mafuta ya chakula yenye ujazo wa lita tano kutoka Sh. 21,000 hadi kufikia 34, 000, huku baadhi ya wananchi wakiamua kutumia mafuta ya ng'ombe kama mafuta mbadala.

Kwa nyakati tofauti jana hadi kufikia majira ya alasiri, baadhi ya wafanyabiashara walikuwa wameanza kurejesha bei ya mafuta hayo ya chakula kama kawaida baada ya kuwapo tishio la kufungiwa leseni.

Juzi, Ole Sabaya akizungumza na wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai katika eneo la Kituo Kikuu cha Mabasi Bomang'ombe, aliwataka wafanyabiashara waliopandisha bei za mafuta ya kupikia, sukari na nyama ya ng'ombe katika msimu huu wa Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, kujitafakari kabla hajazinguana nao.

Mkuu wa Wilaya huyo alisema hakuna tatizo la upungufu wa mafuta nchini isipokuwa wapo wafanyabiashara wakubwa wasiozidi watano, wamekula njama na kukubaliana kupandisha bei ya mafuta ili kupata faida kipindi hiki cha mfungo huo.

"Ninafahamu wala siyo wengi, hawazidi watano na walinunua alizeti yote kutoka kwa wakulima kwa bei ya chini ya soko wakaiweka kwenye kontena na wanaendelea na uzalishaji, isipokuwa wamekubaliana wote wahodhi soko na kupandisha bei ya mafuta," alisema.

Mmoja wa wananchi, Neema Meena, alimweleza Ole Sabaya kuwa mafuta ya kula lita tano yamefikia Sh. 34,000 huku sukari nayo ikipanda kutoka Sh. 2,000 hadi kufikia Sh. 3,000 kwa kilo, jambo alilodai kuwapa wananchi wakati mgumu.

Malalamiko hayo yaliungwa mkono na wananchi karibu wote waliopata nafasi ya kuwasilisha kero zao, wakidai hivi sasa wanalazimika kutumia mafuta ya ng'ombe kupikia na wengine walidai kunywa uji wa futari bila sukari.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kingereka B, Miraji Mkambala, alimweleza Ole Sabaya kuwa wafanyabiashara wa bucha za nyama, wamepandisha nyama ya ng'ombe kutoka Sh. 6,000 na kuuza kati ya Sh. 8,000 na 9,000 kwa kilo.

"Mheshimiwa DC (Mkuu wa Wilaya), sukari kilo moja tulikuwa tukinunua kwa Sh. 2,000 lakini kwa sasa tunanunua kilo 3,000. Jambo hili linatuumiza sisi Waislam na wananchi kwa ujumla, kushindwa kumudu gharama hizo zilizopanda ghafla katika kipindi cha mwezi mmoja.

Kutokana na tatizo hilo, Mkuu wa Wilaya (Ole Sabaya) aliagiza hadi kufikia Aprili 21 (jana), wafanyabiashara wote wa jumla, wawe wamepeleka nyaraka zao kwa maofisa biashara zinazoonyesha bei walizonunulia mafuta hayo na sukari ili kujiridhisha na bei walizonunulia.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, wasipofanya hivyo atapita kila duka na kubandika bei elekezi za bidhaa hizo na atakayeshindwa kuifuata, atamfutia leseni ya biashara.

Kuhusu kupanda kwa bei katika kitoweo cha nyama kutoka Sh. 6,000 hadi Sh. 8,000 mpaka Sh. 9,000, Ole Sabaya aliwataka wafanyabiashara wa bucha kurudisha bei ya awali ya Sh. 6,000.

# Vigogo TANESCO matatani TAKUKURU

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Temeke, imemtia mbaroni Meneja Mwandamizi Uhasibu wa Shirika la Umeme (TANESCO), Philidoni Siyame, kwa tuhuma za kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.4.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa TAKUKURU Temeke, Donasian Kessy, kesi dhidi ya Siyame ilifunguliwa Februari 8 mwaka huu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Alidai Siyame ameisababishia hasara serikali ya kiwango hicho cha fedha kwa kitendo cha kufuta kumbukumbu za upotevu wa vifaa vya umeme kwenye mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za bohari.

Kessy alitaja kesi ya pili yenye namba ECC/12/2021 ambayo nayo ilifunguliwa mahakamani huko Februari 22, mwaka huu, inayomkabili Ofisa Ugavi wa TANESCO, Clemency Mlay, kwa tuhuma za kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 821, akiwa Ofisa Bohari ya Vifaa vya Umeme Kurasini.

Kessy alitaja kesi ya tatu iliyofunguliwa mahakamani huko Februari 3 mwaka huu ilinamhusu Deodatus Joackim (Ofisa Ugavi na Usafirishaji) na wenzake watatu Bernald Inga (Ofisa Ugavi Usafirishaji), Geofrey Maleko (Ofisa Bohari) na Issa Salehe (dereva wa lori) wote watumishi wa TANESCO ambao inadaiwa waliongoza genge la uhalifu kwa lengo la kutenda kosa la wizi kwa watumishi wa umma.

Alidai watuhumiwa wote wanne wameisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 33.08 ambayo ni thamani ya nyaya zenye urefu wa kilomita 17.5.

Kessy alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu, TAKUKURU iliendelea na majukumu yake na ndani ya mkoa huo na ilipokea taarifa 153 zilizohusu vitendo rushwa.

"Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na Kigamboni pamoja na taasisi binafsi zinaongoza kulalamikiwa, jumla ya majalada mapya yaliyofunguliwa na kufikia hatua ya uchunguzi wa kina ni manane na mengine yanaendelea na uchunguzi," alisema.

Alisema katika kipindi hicho, TAKUKURU ilipokea Sh. milioni 16 kutoka katika uchunguzi mbalimbali uliofanyika kupitia SACCOS na fedha za watu binafsi zilizokuwa zimechepushwa au kufanyiwa ubadhirifu.

# Tanzania yashinda kesi Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya juu Marekani imeipa ushindi Serikali ya Tanzania kwa kuitupilia mbali rufani ya Kampuni Vipula D. Valambhia iliyofungua kesi kutaka kukamata mali za Serikali ya Tanzania kutokana na madai ya Dola za Marekani 55,099,171.66.

Uamuzi huo ulitolewa Jumatatu, mahakama hiyo ilitupilia mbali shauri hilo kutokana na kukiukwa kwa taratibu za kimahakama.

Uamuzi wa mahakama hiyo ulibainisha kuwa familia ya mfanyabiashara huyo (Valambhia) ilitaka ilipwe na Serikali ya Tanzania kiasi hicho cha fedha kutokana na mkataba wa ununuzi wa vifaa ulioleta mkanganyiko tangu 1991.

Mlalamikaji katika kesi hiyo alidai kuwa kiasi hicho cha fedha kilipaswa kulipwa tangu Juni 4, 2001 pamoja na riba ya asilimia saba kwa mwaka, hivyo hadi shauri hilo linafikiswa kortini Marekani Februari 2018, madai yalikuwa yamefikia Dola 64,500,750.87.

Hata hivyo, Serikali ya Tanzania kwa muda mrefu imekuwa ikipinga mahakamani malipo hayo dhidi ya Kampuni ya Valambhia. Aprili 2019, Serikali ya Tanzania ilishinda kesi iliyofunguliwa Februari 12, 2018 dhidi ya kampuni hiyo kwenye Mahakama ya Columbia, Marekani.

Walalamikaji katika kesi hiyo walikuwa Valambhia, Pricilla Valambhia, Bhavna Valambhia, Punita Valambhia na Krishnakant Valambhia, ambao ni wajane na watoto wanne wa mfanyabiashara huyo maarufu aliyefariki dunia mwaka 2015 huko Marekani.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Benki ya Tanzania (BoT) na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.


Mudu company limited

## TANGAZO LA MNADA NA NOTISI

Mudu Company Limited, Kwa idhini tuliyopewa na CRDB Bank, tunatoa notisi ya siku kumi na nne kwa wadaiwa/ wamiliki tajwa hapo chini kuwataka walipe madeni yao, na endapo wakishindwa kulipa mali zao zitauzwa kwa mnada wa hadhara kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini;-

| JINA LA MMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA | NAMBA YA KIWANJA | TAREHE YA MNADA/MUDA |
|---|---|---|---|
| NTWARAMANI ADALBERT BAGACHWA | NYUMBA | PLOT NO. 287, BLOCK A, UYOLE AREA, MBEYA CITY | 18/06/2021 IJUMAA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI |
| MARIAM JUWA FANDE MAPUNDA | KIWANJA | PLOT NO. 79, BLOCK G, AMANI GOMVU AREA, KIGAMBONI, DAR ES SALAAM | 25/06/2021 IJUMAA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI |
| MARIAM JUWA FANDE MAPUNDA | KIWANJA | PLOT NO. 77, BLOCK G, AMANI GOMVU AREA, KIGAMBONI MUNICIPALITY | 25/06/2021 IJUMAA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI |
| KHALID SAID SALUM | KIWANJA | PLOT NO. 91, BLOCK G, AMANI GOMVU AREA, KIGAMBONI MUNICIPALITY | 25/06/2021 IJUMAA KUANZIA SAA TANO ASUBUHI |
| MABULA KAYANDA MADUHU | KIWANJA | PLOT NO. 198, BLOCK 6, TUANGOMA AREA, TEMEKE MUNICIPALITY | 25/06/2021 IJUMAA MUDA : SAA NANE MCHANA |
| MIKA ELIA MLONGANILE | NYUMBA | PLOT NO. 37, BLOCK D, KIMBIJI AREA, TEMEKE MUNICIPALITY | 25/06/2021 IJUMAA MUDA: SAA SITA MCHANA |
| MIKA ELIA MLONGANILE | KIWANJA NA FREMU | PLOT NO. 33, BLOCK D, KIMBIJI AREA, TEMEKE MUNICIPALITY | 25/06/2021 IJUMAA MUDA: SAA SITA MCHANA |

**MAMBO YA KUZINGATIA KWENYE MNADA:**

1. Yeyote atakayeshinda mnada kwa kutaja ofa ya juu zaidi kuliko wengine, atatakiwa kulipia 25% ya pesa yote aliyoitaja katika akaunti itayo tolewa na benki mara baada ya kumalizika kwa mnada.
2. Na 75% ya pesa itakayokuwa imesalia, itatakiwa kulipwa ndani ya siku 14 tu kutokea siku ya kufanyika kwa mnada. Ikumbukwe, ikiwa mshindi wa mnada atashindwa kumalizia 75% itakayosalia, hatarudishiwa hata ile 25% ya pesa aliyoilipa awali.
3. Minada yetu inafanywa kwa kuzingatia taratibu za kisheria, hivyo, kwa yeyote atakayejaribu kuharibu minada hii kwa namna yoyote ile, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
4. Kwa mawasiliano zaidi, Piga namba zifuatazo; +255 768 67 23 67.

# Mlipuko aina yake kidato cha kwanza

## ●Wadahiliwa elimu bure rasmi sekondari
## ●CAG: Tujipange miundombinu, walimu

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KILA inapotimu mwezi Desemba, kunasikika wimbo wa serikali uliozoeleka kuhusu elimu shuleni, wanafunzi wanapata fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari na wakati huo huo, wadogo zao nao wanaanza shule, idadi inaongezeka.

Hapo ndipo usemi kwamba 'kila jema na magumu yake' unapotimia, kwani mpango na azma yake ni nzuri, lakini utekelezaji ni mzigo mzito na ikiendewa mahususi kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo iliyopita, wastani wa ongezeko uko juu zaidi kuliko uliozoeleka.

Ndani ya magumu hayo, ya mwaka 2022 yanatarajiwa kuwa na yake ya zaida. Idadi kubwa ya waliodahiliwa kujiunga darasa la kwanza kwa Mpango wa Utoaji Elimu Bila Malipo, wanazalisha kundi la ziada la 'elo wai' (LY) katika kidato cha kwanza ndani ya shule mbalimbali. Mzigo wa ziada kwa serikali; kuu na za mitaa.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), tayari ameshazinyoshea kidole halmashauri nne nchini, kwamba zimo katika orodha ya zinazotarajiwa kubeba mzigo mzito wa ziada kukabili hali hiyo.

### HALI IKOJE?

Mnamo Desemba 5, 2019, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Seleman Jafo, alibainisha kuwa wanafunzi 58,699 (asilimia 7.73) waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza, hawakuchaguliwa kujiunga na elimu hiyo ya sekondari kwa mwaka uliokuwa unafuata (2020) kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Katika mwendelezo wa dosari hiyo, Desemba 17, mwaka jana, Waziri Jafo alitangaza kuwa wanafunzi 74,166 (asilimia 8.9) ya waliofaulu Mtihani wa Taifa wa Darasa la VII, hawakupangiwa shule kwa awamu ya kwanza kutokana na uhaba wa madarasa.

Ubashiri wa kitakwimu, unaibua sura mpya ya ukweli, safari hii huenda siyo ongezeko, bali inapaswa kubatizwa 'mlipuko'. Kwanini? Kwa kurejea Ripoti ya CAG, pia wasilisho la makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) imeshaweka mambo hadharani na kwa maana hiyo yanahitajika maandalizi ya kina ndani ya miezi minane ijayo.

Aliyekuwa CAG, Profesa Mussa Assad, katika Ripoti Mahususi ya Ukaguzi wa Miundombinu ya Shule za Msingi ya mwaka 2017, alikuwa na angalizo la kukosekana uwiano sahihi, kwamba idadi ya wanafunzi inaongezeka kwa kasi maradufu kulinganisha na ongezeko la miundombinu.

CAG Assad alibainisha udahili wa wanafunzi katika shule za msingi nchini uliongezeka kutoka wanafunzi milioni 4.8 mwaka 2001 hadi milioni 8.34 mwaka 2016, akibaini ongezeko la asilimia tano kila mwaka, huku miundombinu ikiwa katika hali mbaya na isiyoendana na idadi ya wanafunzi.

Katika miaka hiyo minne iliyopita, mkaguzi hiyo wa kitaifa aliainisha idadi ya wanafunzi kwenye shule za msingi nchini ilikuwa milioni 8.34 kwa shule za serikali na madarasa yao yalikuwa 108,448, ambayo ni wastani wa nusu (asilimia 52) ya mahitaji halisi ambayo ni madarasa 208,540.

Pia, kwa kutumia kigezo hicho, imaanisha kulikuwa na ukiukwaji wa kanuni za ufundishaji bora, unaohitaji darasa liwe na wanafunzi wasiozidi 45, lakini kulinganisha



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu.

na hali ilivyokuwa, darasa moja lilisheheni wanafunzi 77, ambayo inakaribia kuwa sawa na madarasa mawili.

"Ukaguzi ulibaini kuwa, katika miaka mitano mfululizo kuanzia 2011/12 hadi 2015/16, wastani wa wanafunzi milioni 3.73, sawa na asilimia 48 hawakuwa na maisha mazuri ya darasani yanayohitajika ili kukidhi misingi ya elimu bora kwa shule za msingi," CAG alibainisha.

Alifafanua kuwa mwaka 2012, wanafunzi milioni 3.53 walidahiliwa kujiunga na shule za msingi ambazo hazikuwa na madarasa na utaratibu huo uliendelea katika miaka iliyofuata kukiwa na ongezeko hilo la wastani wa asilimia tano kwenye udahili kwa miaka mitano mfululizo.

Kwa maana hiyo, wakati mwaka 2016 kulivyoshuhudiwa mlipuko wa udahili ambao ulielemea uhalisia wa mahitaji kutokana na serikali kuanza kudahili pasipo malipo (elimu bure), tayari miaka mitatu kabla, jahazi hilo lilikuwa limeanza kuelemewa.

Vilevile, katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20 iliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma hivi karibuni CAG, Charles Kichere, anabainisha kuwapo upungufu wa madarasa na mazingira miundombinu duni katika utoaji wa elimu ya msingi na sekondari nchini.

CAG anabainisha kuwa upungufu ulipimwa kwa kuzingatia uwapo wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na madawati katika shule za msingi na sekondari.

Anabainisha kuwa ukaguzi na uchambuzi wa takwimu zilizopo ulibainika kulikuwa na wanafunzi milioni 10.11 ambao waliandikishwa katika shule za msingi za umma wakati vyumba vya madarasa vilivyokuwapo nchini kote vilikuwa 118,255 badala ya 252,791 hadi kufikia mwaka 2018.

CAG Kichere anabainisha kuwa hali ni mbaya zaidi katika Halmashauri za Mbulu, Mpwapwa, Mpanda na Geita, akibainisha kuwa kwenye miundombinu ya vyoo zina upungufu wa kuanzia asilimia 73 hadi 75, hali iliyosababisha kuwa na wastani wa uwiano wa 1:55 badala ya 1:25.

"Sera ya elimu ya msingi bila malipo iliyoanzishwa mwaka wa fedha 2015/16 imepelekea ongezeko la haraka la idadi ya watoto wanaoandikishwa darasa la kwanza.

"Uandikishaji wa darasa la kwanza umeongezeka kwa kiasi kikubwa na kusababisha msongamano katika madarasa, hivyo kuleta uhitaji mkubwa kwenye miundombinu mingine ya shule.

"Pia, kuna ongezeko kubwa la idadi ya watoto wanaostahili kudahiliwa kutoka shule za msingi kwenda sekondari kila mwaka. Nyongeza hii ya uandikishaji shuleni inatakiwa kwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya shule, CAG Kichere anapendekeza katika ripoti yake hiyo.

Anabainisha kuwa alifanya tathmini ya utoshelevu wa miundombinu ya elimu za msingi na sekondari katika halmashauri 51 na kubaini kulikuwa na upungufu mkubwa wa miundombinu ya shule kama vile madarasa, ofisi, mabweni, maabara, vyoo, kumbi za chakula, madawati, meza, viti na nyumba za watumishi.

"Upungufu wa miundombinu huleta athari katika ubora wa elimu. Ninapendekeza kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI kuchukua hatua zinazorekebisha au kutokomeza tatizo la upungufu wa miundombinu ya shule ili kuimarisha ubora wa elimu nchini," CAG anashauri

### DIRA YA HAKIELIMU

Ndani ya mtazamo wa ubashiri kama wa CAG, asasi ya HakiElimu nayo ina angalizo kama hilo, ikihusu ongezeko la idadi ya wanafunzi, walimu wao, miundombinu inayowahusu na hususan madarasa na vyoo, vitabu na huduma ya ruzuku ya elimu bure.

Mkuu wa Programu wa HakiElimu, Godfrey Boniventura, anatahadharisha hitaji hilo litakalokuwa rasmi miezi minane ijayo analolibatiza kwa jina la 'bomu', akioanisha mlipuko huo kwa kigezo cha takwimu ya idadi ya wanafunzi wa mwaka 2015 na wastani wa ongezeko lao la kila mwaka.

Kwa mujibu wa Ofisa Programu huyo, udahili wa kidato cha kwanza mwakani pia una sura mpya ya nyongeza, kwamba ni sehemu ya zao la wanufaika wa udahili wa darasa la kwanza wa elimu bure mwaka 2016.

Boniventura anasema uchambuzi wao wa takwimu za udahili umebaini kuwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, idadi ya wanafunzi wanaoingia kidato cha kwanza itaongezeka hadi kufikia wanafunzi 1,882,500, hivyo kuongeza pia mahitaji ya madarasa, walimu, vitabu, vyoo na ruzuku ya elimu bure.

Anabainisha kuwa kutokana na idadi hiyo kutahitajika madarasa 41,833, akibainisha kuwa kwa sasa shule za sekondari zinakabiliwa na uhaba wa madarasa 4,647, hivyo inafanya uhitaji wa madarasa uwe mkubwa zaidi kufikia madarasa 46,480.

Boniventura anasema matundu ya vyoo 75,000 yatahitajika, vitabu milioni 18.825, walimu 41,833 na Sh. bilioni 47 kila mwezi kwa ajili ya ruzuku ya elimu bure. Kwa sasa, serikali inatoa Sh. bilioni 23 kila mwezi kugharamia mpango huo.

Kwa kutambua uzito wa suala hilo, asasi za taasisi zilizokutana mjini Dodoma Jumatatu katika warsha ya kujadiliana masuala mbalimbali yanayogusa sekta za elimu, maji, kilimo na afya, ziliazimia kuandikia barua Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuishauri kutenga fungu mahususi kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari na kuajiri walimu wapya.

Warsha hiyo iliandaliwa na Taasisi ya WAJIBU ikishirikisha asasi na taasisi za serikali zikiwamo HakiElimu, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Bunge, The Foundation for Civil Society (FCS), ANSAF, Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na TACOSODE.

Meneja Fedha na Utawala wa WAJIBU, Jackson Mmary, alisema wataandika barua kwenda Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kuishauri serikali kuchukua hatua kuajiri walimu na kuongeza miundombinu ya shule za sekondari nchini kukabiliana na kasi ya ongezeko la wanafunzi.

### MIKAKATI YA SERIKALI

Akiwasilisha bungeni juzi makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya RAIS -TAMISEMI, Ummy Mwalimu, alisema serikali imepanga kuanza kujenga shule mpya 300 za sekondari za kutwa kwenye kata ambazo hazina shule za sekondari kwa gharama ya Sh. milioni 650 hadi 700 kwa kila shule kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari.

Ummy alisema kuwa katika mwaka ujao fedha, serikali itaanza kutekeleza awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule 10 kati ya 26 za sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi (shule moja kwa kila mkoa) ambapo katika awamu hiyo ya kwanza itajengwa miundombinu ya kidato cha tano na sita.

Alisema shule hizo zitakapokamilika zitakuwa na kidato cha kwanza hadi cha sita, zikiwa na uwezo wa kupokea wanafunzi kati ya 1,000 hadi 1,200 kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP), serikali ikitenga Sh. bilioni 40 kuugharamia.

Vilevile, alisema kutakuwa na ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa 1,840 ya shule za sekondari kwa gharama ya Sh. bilioni 23, kujenga nyumba 300 za walimu kwa gharama ya Sh. milioni 50 kwa kila nyumba.

Alisema wizara itaendelea kugharamia Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo, zikitengwa Sh. bilioni 312.05 (fedha za ndani) huku serikali ikipanga kutumia Sh. bilioni 50 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya shule za msingi na sekondari.

## Majibu DNA yachelewesha kesi ya Padri

**Na Daniel Sabuni,** HAI

MAJIBU ya vipimo vya sampuli za vinasaba (DNA) ya Padri Erasmus Swai (44) anayekabiliwa na kesi ya kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne, jana yaliikwamisha kutolewa katika Mahakama ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, kuendelea kusikiliza shauri hilo.

Padri Swai kabla ya kushtakiwa kwa kesi hiyo, alikuwa Paroko wa Parokia ya Manushi ya Jimbo Katoliki la Moshi.

Jana, Hakimu Mkazi Thurston Kombe anayesikiliza kesi hiyo, aliahirisha shauri hilo hadi Mei 5, mwaka huu, itakapoendelea kusikilizwa. Mahakama ilishindwa kuendelea kusikiliza shauri hilo, baada ya majibu hayo ya DNA kudaiwa kuchelewa kuwasilishwa mahakamani.

Upande wa mashtaka, ulilazimika kufanya vipimo kwa DNA, kwa Padri anayedaiwa kuwa baba wa mtoto huyo na mtoto aliyezaliwa, ambaye ana umri wa miezi sita sasa. Sampuli hizo zilichukuliwa mwezi mmoja na majuma mawili yaliyopita, kutokana na amri ya mahakama. Kabla ya kuahirishwa kwa kesi hiyo jana, Mwendesha Mashtaka wa Serikali Lobulu Mbise, alidai mahakamani hapo kuwa vipimo vya sampuli za vinasaba vimechelewa.

Alidai mahakama hapo kwamba badala ya siku 42 zilizokubaliwa kwa utaratibu wa Mkemia wa Serikali wa Kanda ya Arusha, sasa majibu yamechelewa kutoka na kufikia siku 46.

Padri Swai anadaiwa kutenda makosa hayo kwa mtoto mwenye umri wa miaka 17, ambaye alikuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kimaseki iliyoko mkoani Arusha.

Katika hati ya mashtaka, inadaiwa kuwa Machi, mwaka jana, katika Hoteli ya Snow View iliyoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bomang'ombe, kwa nyakati tofauti, Padri Swai alimbaka mwanafunzi huyo.

Pia ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitenda makosa mawili, la kwanza ni kubaka chini ya kifungu cha 130 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 2002, na kosa la pili ni kumpa mwanafunzi ujauzito, chini ya kifungu cha 60 (a) cha Sheria za Elimu.



Kinamama wa kikundi cha Jipe Moyo cha Kijiji cha Kome, jimbo la Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakiandaa shamba lao juzi, kwa kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe ambalo ni miongoni mwa yale yaliyogawiwa bure na Mbunge wa jimbo hilo, Prof. Sospeter Muhongo (hayupo pichani), kwa vikundi mbalimbali vya wakulima jimboni mwake. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Samia awaondoa hofu wawekezaji wa China

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amekutana na viongozi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa China nchini Tanzania (Chinese Business Chamber of Tanzania) na kuwahakikishia kuwa serikali itafanyia kazi changamoto mbalimbali zinazokwamisha uwekezaji nchini.

Pia, serikali imewaahidi kushughulikia upatikanaji mgumu wa vibali vya kazi, kodi, ucheleweshaji wa malipo, urasimu, kushughulikia changamoto zinazojitokeza kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Taarifa iliyotolewa naa Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, IKULU, Gerson Msigwa, ilisema

viongozi hao wakiongozwa na Janson Huang, wamempa pole Rais Samia kutokana na msiba wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli na kumpongeza kwa kupokea kijiti cha urais katika Serikali ya Awamu ya Sita.

Pia, wamemhakikishia kuwa wafanyabiashara wa China wapo tayari kushirikiana na serikali katika kukuza uchumi na kuinua ustawi wa wananchi kwenye uwekezaji mkubwa wanaokusudia kuufanya kupitia kampuni zaidi ya 800 za China zilizo tayari kuwekeza Tanzania.

Wametaja maeneo ambayo kampuni zao zipo tayari kuwekeza kuwa ni viwanda vya kutengeneza simu, dawa za binadamu, magari, kuanzisha maeneo maalum ya viwanda (Industrial Parks) na kuwawezesha Watanzania kupata ujuzi kupitia mpango wa elimu utakaotoa fursa kwa Watanzania kusoma vyuo vya Tanzania na China katika masuala mbalimbali yakiwamo uhandisi na utalii kwa ufadhili wa Serikali ya China na Jumuiya ya Wafanyabiashara wa China.

Akizungumza na viongozi hao, Rais Samia aliwashukuru kwa salamu zao za pole na pongezi na amewahakikishia kuwa serikali yake itashirikiana nao katika uwekezaji na kuboresha zaidi mazingira ya biashara na uwekezaji ili matokeo ya uwekezaji huo yanufaishe pande zote mbili.

Aliwahakikishia kuwa serikali itafanyia kazi changamoto mbalimbali zinazokwamisha uwekezaji ikiwamo upatikanaji mgumu wa vibali vya kazi, kodi, ucheleweshaji wa malipo, urasimu, kushughulikia changamoto zinazojitokeza kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa korona (Covid-19).



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# NEC isikubali madai haya kuiharibia taswira

**KUNA** malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa mara kwa mara katika siku za karibuni, kuhusiana na namna wasimamizi wasaidizi na makarani katika vituo vya kupigia kura wanavyopatikana.

Kwamba wengi wamekuwa wakipewa nafasi hizo kwa upendeleo bila kufuata vigezo na sifa za wahusika pale zinapotokea nafasi hizo wakati wa uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo.

Imekuwa ikidaiwa kuwa upendeleo huo umekuwa ukizingatia itikadi za vyama vya siasa, udugu, urafiki na mambo mengine yanayofanana na hayo, ambayo ni aibu na fedheha kwa taifa.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ambayo ndicho chombo chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo katika majimbo na kata, haikuwahi kutoa ufafanuzi kuhusiana na malalamiko hayo.

Hata hivyo, mapema wiki hii, mmoja wa makamishna wa NEC, Omar Ramadhani Mapuri, aliligusia suala hilo na kuonyesha kwamba lina ukweli ndani yake.

Kutokana na hali hiyo, Mapuri aliwataka wasimamizi wa uchaguzi ndogo za ubunge na udiwani kuacha kuweka ndugu na jamaa zao katika vituo vya kupigia kura kwa ajili ya kusimamia kusimamia ili kuondoa malalamiko.

Mapuri alitoa kauli hiyo na kutoa angalizo dhidi ya malalamiko hayo wakati akifungua mafunzo ya watendaji wa chaguzi ndogo katika kanda tatu wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga.

Alisema kuwa kuweka ndugu au jamaa kwenye usimamizi wa vituo vya chaguzi kunasababisha athari kwa kuwa ni vigumu kuwachukulia hatu wanapoharibu kazi.

Aliwataka watendaji hao kuzingatia sheria na taratibu za uchaguzi katika maeneo yao na kufahamu jiografia ya sehemu unapofanyika uchaguzi.

Kwa mujibu wa kamishna huyo, watendaji hao wameaminiwa kwa kuwa wana uwezo, wanajiamini na kujitambua, hivyo NEC ina imani uchaguzi utafanyika vizuri bila kuwa na dosari yoyote na kuhakikisha hakutakuwa na malalamiko yoyote kutoka kwa wananchi na vyama vyote vya siasa vitakavyoshiriki.

Kama kamishna hiyo wa tume ameiona dosari hiyo, bila shaka NEC kama chombo chenye dhamana ya uchaguzi itakuwa imeliona jambo hilo kuwa ni tatizo na kikwazo katika dhana nzima ya uchaguzi huru na haki.

Hata hivyo, tunapata wasiwasi kama chombo hicho kitaweza kulitatua tatizo hilo, kutokana na kasoro za muundo wake ambazo wadau wa uchaguzi wamekuwa wakizieleza na kutaka kuwapo kwa tume huru kila uchao.

Tunaliona hilo kwa sababu NEC haina watumishi wake wa kusimamia uchaguzi, badala yake inawatumia mawakala (wakurugenzi wa halmashauri), ambao ni watendaji wa serikali walioteuliwa na rais anayetokana na chama tawala.

Kwa msingi huo, wakurugenzi hao kwa kuwa wanawajibika kwa mamlaka ya uteuzi wao, hawanabudi kutekeleza majukumu yao kwa kufuata maelekezo ya wateule wao.

Tunaishauri NEC kutafuta namba ya kushughulikia tatizo hili ili kulinda tawira yake kwa umma na wadau wa uchaguzi kwa ujumla, vinginevyo inaweza kutokuaminika kwa uamuzi wowote inaoufanya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Trafiki nawapongeza, ila la spidi kamera kubambikwa, mjitafakari

Na Beatrice Shayo

KUNA ukweli usiopingika, Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kushirikiana na wadau wenzao, wamejitahidi kwa kiasi kikubwa kupunguza ajali za barabarani nchini.

Tumeona jitihada zao ikiwamo kutoa elimu kuhusiana na usalama barabarani, madereva wameelimishwa kuzingatia sheria zinazowahusu, kupunguza janga la ajali.

Kwa kutumia ukweli wa takwimu zinazotolewa na wahusika, wanafunzi na watembea kwa miguu sasa ni werevu wa kutumia alama zilizowekwa za pundamilia na mengine mengi wanapovuka barabara kwa usalama, leo hii matunda yanaonekana kwa kupungua ajali kitaifa.

Ajali hizo zimeshasababisha madhara makubwa, kwani wako watu waliopoteza maisha, kujeruhiwa, kupoteza mali na wengine kupata ulemavu wa kudumu.

Takwimu mbalimbali zinaonyesha vifo vingi barabarani, chanzo kikuu ni uzembe wa madereva wasiozingatia sheria za usalama barabarani. Hapo nawapongeza sana.

Ila niseme, licha ya mafanikia na mikakati mingi iliyowekwa, bado kuna yanayotia doa utendaji wa baadhi ya askari hao wa usalama barabarani, mahsusi nikielekea mikoa ya Kaskazini mwa nchi.

Kuna tabia nisiyoipenda. Huwa wanakuamuru dereva kuegesha gari pembeni kando wakidai umezidisha kiwango cha mwendokasi kinachostahili na unapomuelewesha, askari anakuambia ushuke na kuvuka barabara kumfuata.

Unapofika aliko, anaanza kukudadisi kulikoni mwendokasi huo na unapomkana kwa unachoaminii, hakubaliani nawe. Ukikagua kifaa unakuta mwendesha gari yuko sahihi, hajazidi spidi 50. Hapo unajikuta unabaki na maswali "ina maana 'dash board' imeanza kushindwa kusoma kilometa au nini kimetokea hapo?" Unatamani kumuuliza fundi wako nini kimetokea, ila ndio hivyo, mazingira si rafiki.

Askari anabaki kakutolea macho, huku akikutamkia "nakuandikia kosa umezidisha mwendo." Unapojitetea "mbona sijazidisha mwendokasi' anakujihu "unataka kubishana na tochi?" dereva unabaki na mawazo.

Kila unapojaribu kujitetea, askari hataki kukuelewa. Hapo anakuacha ukibisha, mwenyewe anaenda kuongea na dereva mwingine aliyekamatwa na akimaliza huko, anakurudia katika namna anakuchukulia unampotezea muda, licha ya kwamba unadadisi ukweli.Sasa inapokuja kwenye kipengele cha kutaka akuonyeshe gari ilipozidisha spidi katika kamera zao, ataanza kukuambia "ina maana huamini ninachokuambia? Umezidisha mwendo!"

Ukiendelea 'kukomaa' utaona anaanza kuitafuta picha ya gari na swali atakalokuambia 'taja namba ya gari yako', huku akiendelea kuitafuta na baada ya muda anakuambia "uondoke haipo sasa."

Najiuliza, kama haipo picha, amepata wapo dai la kasi kubwa ya gari alilolikamata? Anakuwa kakupotezea muda zaidi ya dakika nusu saa.Ukijitahidi kujielelezea, hakutaka kukusikiliza. Anakazania "nakuandikia kosa la spidi, halafu akishindwa hoja anakuambia 'tembea." Nadhani hilo halijakaa sawa.

Wakati mwingine unakamatwa na ukidai picha, unajikuta anakuonyesha ya gari lingine na pale unapohoji mbona hizo namba sio ya gari unaloendesha, anakuambia uondoke.

Ni vyema mtu anapokamatwa kwa kuzidisha mwendokasi wa gari lake, bado vyema afahamishwe kosa lake mara moja, badala ya kuzungushwa mara 'paki gari kwa mbele' na kwenda kuvuka barabara kumbembeleza askari, wakati hujafanya kosa.

Hapo ndipo baadhi ya madereva wanashuhuduwa na hadithi za kutoa rushwa pasipo kujua kosa lao, hasa kwa wasio na ujasiri kudai picha ya gari.

Kwanini wanapodaiwa picha ya kasi hiyo, wanakuwa wakali kama mbogo. Utasikia askari anahoji, "inamaana hutuamini, lete leseni tukuandikie kosa lako la kuzidisha mwendo!" Hivi ni kipi kinachowafanya askari trafiki muwe wakali wakati ni haki ya dereva kuonyeshwa spidi yake, badala ya kumtajia kwa mdomo. Askari unapomtajia mtu alikuwa spidi 70 sehemu ya mwendo wa 50, muonyeshe katika kamera yako ashuhudie kosa lake.

Wengine anakutaji ulikuwa spidi 70 kwa saa, kwenye kibao kinachomtaka dereva awe mwendo spidi 50. Ukicheki, unakuta umezingatia maelekezo ya kibao na ukimtaka akuonyeshe picha ndio balaa, ndio penye sinema inanaza kutafuta hilo gari.

Busara ni hakuna haja ya kumbambikia spidi dereva, busara mueleze kosa lake kama linavyosoma kwenye kamera zenu na kama kosa, hakuna haja ya kumpotezea muda wake.

TANGAZO

# TPB BANK PLC

Tpb Bank
Grow with us

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA [MAHESABU YALIYO KAGULIWA]

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### TPB BANK PLC
### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA, 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | | Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Mwaka uliopita 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 41,717 | 37,749 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 19,080 | 25,827 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 100,455 | 100,588 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 114,106 | 7,946 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 5 | 4 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 85,732 | 6,611 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 617,814 | 420,594 |
| | 12 | Mali Nyingine | 33,187 | 16,789 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 22,951 | 21,891 |
| | | Haki ya matumizi ya mali | 8,633 | 9,186 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,043,679** | **647,184** |
| B | | **DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| | 18 | Amana za Wateja | 676,665 | 442,177 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 | Amana Maalumu | 126,420 | - |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 5,951 | 1,096 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2 | - |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 14,972 | 4,126 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | 2,825 | 2,054 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 21,596 | 15,952 |
| | | Dhima ya kukodisha | 6,211 | 7,314 |
| | 28 | Madeni | 84,738 | 75,572 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **939,380** | **548,291** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **104,299** | **98,893** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 60,667 | 44,710 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 5,866 | 15,891 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 9,694 | 10,220 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **104,299** | **98,893** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 89,979 | 25,132 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 17,370 | 19,306 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 44 | 70 |
| D. | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.99% | 15.28% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 14.09% | 5.67% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 79.53% | 85.61% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 59.20% | 64.99% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 77.04% | 81.55% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 53.03% | 13.20% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | 61.26% | 15.09% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Limbikizo la Mwaka Wa Sasa 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 122,171 | 100,177 |
| 2 | Gharama za Riba | (37,359) | (22,496) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **84,811** | **77,681** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (8,420) | (10,533) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **32,740** | **29,539** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 2,339 | 2,074 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 19,828 | 20,851 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 10,572 | 6,614 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(88,123)** | **(73,680)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 40,802 | 35,719 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 399 | 526 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 46,921 | 37,436 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **21,008** | **23,006** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 15,142 | 7,115 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **5,866** | **15,891** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | **66** | **133** |
| | 11.1 Hasara ya sasa kutoka kwa wajibu wa faida | 95 | 190 |
| | 11.2 Kodi kadirio la mbeleni la mafao ya mtumishi | (28) | (57) |
| | 11.3 Gharama ya zamani juu ya wajibu wa faida | - | - |
| | 11.4 Kodi iliyopungua kwa gharama ya zamani kwenye wajibu unaofafanuliwa | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **5,932** | **16,024** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 1,039 | 926 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 211 | 571 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 43 | 38 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.70% | 2.65% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 5.84% | 17.63% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 56.89% | 56.80% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 10.03% | 12.84% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA, 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Limbikizo la Mwaka wa 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi [Mwaka Uliopita] 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 21,008 | 23,006 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali | 10,122 | 13,756 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (199,157) | (9,325) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (1) | 2 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 360,908 | 51,578 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (91,189) | (32,321) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 22,131 | (4,417) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (17,717) | 3,271 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (7,819) | (6,900) |
| | - Kodi kadirio la mbeleni la mafao ya mtumishi | (861) | (490) |
| | - Gharama ya mafao ya mtumishi | 1,088 | 1,091 |
| | - Mengineyo (Mapato ya ruzuku & hifadhi nyingine) kutoka muunganiko wa biashara ) | (94) | (42) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***98,421*** | ***39,210*** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (4,502) | (4,001) |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoonekana | (208) | (1,409) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 2 | 1 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | ***(4,708)*** | ***(5,410)*** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | (1,210) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 612 | 888 |
| | Malipo ya Dhima ya Kukodisha | (7,545) | (4,992) |
| | Mengineyo (Kodi katika Hisa za Ziada) | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | ***(6,932)*** | ***(5,314)*** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **86,780** | **28,487** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 33,746 | 5,260 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **120,526** | **33,746** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA, 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo [bainisha] | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **60,601** | **(0)** | **0** | **10,220** | **98,893** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | 4,048 | (135) | (3,913) | - | - |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya | - | - | 5,866 | - | - | - | **5,866** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 66 | - | - | - | **66** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yalifafanuliwa baada | - | - | - | - | - | - | - |
| Kodi ya faida ya mtaji wa TWIGA & TWB | - | - | - | - | - | (107) | **(107)** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (419) | **(419)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **70,581** | **(135)** | **(3,913)** | **9,694** | **104,299** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **40,539** | **135** | **3,913** | **10,262** | **82,920** |
| Mabadiliko ya IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya udhibiti | - | - | 4,048 | (135) | (3,913) | - | - |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya | - | - | 15,891 | - | - | - | **15,891** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (1,210) | - | - | - | **(1,210)** |
| faida ya sasa ya manufaa yalifafanuliwa | - | - | 133 | - | - | - | **133** |
| Kurudishwa kwa Gawio lililosimamishwa mwaka | - | - | 1,200 | - | - | - | **1,200** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (42) | **(42)** |
| Salio la mwisho wa mwaka | **28,072** | - | **60,601** | **(0)** | **0** | **10,220** | **98,893** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA, 2020

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **MR. SABASABA K. MOSHINGI**<br>(Ofisa Mtendaji Mkuu) | | **29.03.2021** |
| **MS. REGINA E. SEMAKAFU**<br>(Mkuu wa Fedha) | | **29.03.2021** |
| **MR. SOSTHENES F. NYENYEMBE**<br>(Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | | **29.03.2021** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA**<br>Mwenyekiti wa Bodi | | **29.03.2021** |
| **MS. ANNE C. MBUGHUNI**<br>Mjumbe wa Bodi | | **29.03.2021** |
| **MR. GILBERT W. CHAWE**<br>Mjumbe wa Bodi | | **29.03.2021** |

Head Office: LAPF Towers Bagamoyo Roard. P.O. Box 9300 Dar es Salaam Tanzania. Telephone: +255 22 2162940, Fax: +255 22 2114815, Email: info@tpbbank.co.tz

# Kaya zahimizwa kuanzisha miradi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Erasto Makala amewataka watu walio katika kaya masikini zitakazoingia kwenye utekelezaji wa sehemu ya pili ya mpango wa kuzinusuri kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) awamu ya tatu, kuibua miradi ya miundombinu.

Makala alitoa wito huo juzi wakati wa kikao cha siku moja cha kujenga uelewa kuhusu kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF na kutoa mwongozo wa utambuzi na uandikishaji wa kaya za walengwa katika eneo la utekelezaji kilichofanyika Mlandizi. Kikao hicho kiliwashirikisha madiwani, wakuu wa idara na wawezeshaji.

Alisema katika awamu iliyopita, kuna miradi ilitekelezwa ikiwamo wa lambo la maji Lukenge na Magindu ambayo imekuwa imeondoa kero iliyokuwapo awali.

Kaya zitakazoingia kwenye mpango katika awamu hii, alisema zinatakiwa kuibua ubovu wa miundombinu katika maeneo yao hususani barabara.

"Nawashukuru TASAF kwa lengo lao la kunusuru kaya masikini. Nawaomba katika awamu hii pia wajikite katika miundombinu ya vyumba vya madarasa kwani naamini wataendelea kufanya mambo makubwa kuliko awali na kaya za walengwa zitafanya kazi kwa bidii kujiongezea kipato," alisema Makala.

Naye Diwani wa Viti Maalum, Josephine Gunda, alisema kaya zilizonufaika katika awamu iliyopita zimekuwa na mabadiliko kiuchumi. Aliomba idadi ya kaya za wanufaika iongezwe kwa kuwa walioachwa awali walikuwa wengi.

Akizungumza niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ofisa kutoka katika Mfuko huo Zuhura Mdungi, alisema utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya masikini pia umewezesha kaya za walengwa kujikita kwenye shughuli za kukuza kipato na kujiimarisha kiuchumi ikiwamo ufugaji, uvuvi, kilimo na biashara.

Mdungi alisema katika kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF kitafikia zaidi ya kaya 1,450,000 zenye zaidi ya watu milioni saba nchini kote ikiwa ni nyongeza ya kaya 350,000.

Alisema mpango huo utawezesha kaya masikini zinazoishi katika hali duni hususani watoto na akina mama wajawazito kupata lishe bora, husuma za afya na Elimu.

# Wananchi waipeleka halmashauri kortini

**Na Richard Makore,**
MWANZA

ZAIDI ya wananchi 143 wa Luchelele wilayani Nyamagana, wameipeleka kortini Halmashauri ya Jiji la Mwanza katika kesi ya mgogoro wa ardhi iliyokuwa inasikilizwa Mahakama Kuu ya Tanzania kitengo cha biashara kanda ya Mwanza.

Katika kesi hiyo wananchi hao wanapinga kuhamishwa kutoka maeneo yao na kulipwa Sh. milioni moja kwa kila kiwanja kimoja ambacho Halmashauri ya Jiji la Mwanza ingepima.

Baada ya kesi hiyo kunguruma kwa kipindi kirefu, pande zote mbili zilikubali kufanya makubaliano ya kisheria na kutakiwa kutekelezwa na halmashauri hiyo, lakini mpaka leo wamekaidi kuyatekeleza.

Akizungumza mahakamani hapo jana jijini Mwanza, mwakilishi wa wananchi hao, Fortunatus Maiga, aliomba mahakama hiyo mbele ya Jaji James Karayemaha, kuagiza halmashauri hiyo itekeleze makubaliano hayo ya kisheria yaliyofikiwa Julai 15, 2016.

Aliiambia mahakama kuwa wakati kesi hiyo ya msingi ikiendelea wamekuwa wakipokea maelekezo mengine kutoka kwa viongozi wa serikali ambayo yanakiuka sheria.

Jaji Karayemaha wa mahakama hiyo, alipanga Mei 20, mwaka huu kwa ajili ya kutoa uamuzi wa kukazia hukumu kuhusu makubalino ya pande zote mbili.

Hata hivyo, wawakilishi wa halmashauri hiyo hawakuwapo mahakamani hapo ili kusikiliza kesi hiyo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Suleiman Jafo, akibadilishana mawazo na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, baada ya kuzungumza na waandishi wa habari, kuhusu kukamatwa kwa shehena ya vifungashio vya plastiki jijini Mwanza jana. **PICHA: OMR**

# Waliokamatwa na shehena mifuko ya plastiki matatani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ameagiza kuchukuliwa hatua kali kwa watu waliokamatwa na shehena ya vifungashio vilivyopigwa marufuku na serikali.

Jafo alitoa agizo hiyo jana baada ya kushuhudia magunia 40 na katoni 16 za vifungashio hivyo ambavyo havina ubora vilivyokamatwa wakati wa msako uliofanywa Soko Kuu la Jiji la Mwanza.

Akizungumza baada ya kushuhudia shehena hiyo iliyohifadhiwa katika Kituo Kikuu cha Polisi wilayani Nyamagana baada ya kukamatwa, Waziri Jafo aliwapongeza watendaji wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), uongozi wa mkoa, Wilaya ya Nyamagana na Jeshi la Polisi kwa ushirikiano wao. Waziri huyo alisema kuwa endapo vifungashio hivyo visingekamatwa, vingesambaa mitaani na kutumiwa na walaji na kuendeleza uchafuzi mkubwa wa mazingira, hivyo kurudisha nyuma kampeni ya kupiga marufuki mifuko na vifungashio visivyo na viwango.

"Serikali ilishatoa tamko kuwa mwisho wa vifungashio hivi ni Aprili 8 na mimi nilitolea tamko Aprili 8, sasa kuna baadhi ya watu wasio na nia njema wanaendelea kusambaza mifuko hii, sasa nina imani watafikishwa haraka mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake," alisisitiza.

Alisema serikali imekuwa ikitoa maelekezo lakini wapo baadhi ya watu wanakaidi, hivyo itaendelea kuhakikisha maelekezo yote inayotoa yanafanyiwa kazi na vilevile haitavumilia wanayoyakaidia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, alisema ushirikiano wa pamoja kati ya vyombo vya dola na taasisi zingine ikiwamo NEMC ndiyo umeleta mafanikio hayo.

Aliushukuru uongozi wa Wilaya ya Nyamagana pamoja na NEMC kwa kufuatilia na jukumu la jeshi hilo ni kuhakikisha sheria zote zilizotungwa na Bunge zikiwamo zinazohusu masuala ya mazingira zinatekelezwa.

Aliongeza kuwa wataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo wanaojihusisha na biashara ya mifuko na vifungashio vilivyokatazwa wanakamatwa.

Kamanda huyo aliahidi kushirikiana na Ofisi ya Mashtaka ambayo iko kisheria kuhakikisha mwenendo wa kesi unakwenda vizuri na baadaye kupata matokeo mazuri.

Meneja wa NEMC wa Kanda ya Ziwa, Redempta Samuel, aliwataka wananchi kuacha mara moja kutumia mifuko na vifungashio vilivyopigwa marufu na serikali ili kuepuka madhara.

"Sasa ni wakati mwafaka wa kuacha kutumia mifuko na vifungashio hivi kwa faida yetu wenyewe kwani vinaleta madhara, vinaziba mifereji, wanyama wanakufa, tukiichoma ule moshi wenye kemikali unatudhuru, hebu tutumie mifuko mbadala kuepuka mgogoro na serikali," alisema.

Katazo la mifuko ya plastiki linataja makosa matano ya kuzalisha, kuingiza, kusambaza, kuuza na kutumia mifuko iliyokatazwa na adhabu yake ni faini ya kuanzia Sh. 30,000 hadi bilioni 10 au kifungo hadi miaka miwili.




Kamishna wa Ushirikishwaji Jamii Jeshi la Polisi, CP Dkt. Mussa Ally Mussa (wa tatu (kulia)) akionesha nakala za Mwongozo wa Kuzuia Uhalifu kwa Polisi Kata/Shehia na Maafisa Watendaji wa Kata/Shehia, Mitaa na Vijiji. Wengine ni Msemaji wa Jeshi la Polisi, SACP David Misime (wa pili -kushoto), Mkurugenzi wa Miradi DataVision International, Macmillan George (wa tatu-kushoto); Msimamizi wa Kitengo Cha Ushirikishwaji Jamii SACP Engelbert Kiondo (wapili kulia) na kulia ni Afisa Msaidizi kitengo cha Ushirikishwaji Jamii, Inspekta Issa Asali. **NPUGAPUCHA WETU**

# MCT yataka watendaji wanyanyasaji waanikwe

**Na Somoe Ng'itu**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limewataka waandishi wa habari nchini kutoa taarifa za kunyanyaswa na viongozi mbalimbali wa serikali na taasisi binafsi endapo watakutana na madhila hayo wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam wakati akifunga semina ya waandishi wa habari kutoka mikoa mbalimbali jana, Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema baraza linahitaji kupata ushahidi wa matukio hayo na kuyafanyia kazi kwa malengo ya kukomesha vitendo hivyo.

Mukajanga alisema baraza haliwezi kushughulika na kadhia hiyo kwa vitendo endapo waandishi husika watashindwa kuwasilisha taarifa rasmi na hatimaye kulimaliza tatizo hilo.

"Tunafahamu tatizo ni kubwa, ila sisi tunahitaji ushahidi kutoka kwenu, bila nyinyi kutusaidia kupata ushahidi wa madhila hayo, hatutaweza kuyafanyia kazi kikamilifu, leteni taarifa kutoka katika wilaya zenu, tarafa na kote zinapotokea," alisema Mukajanga.

Katibu huyo aliwataka waandishi waliopata mafunzo, kwenda kuyatoa kwa wenzao ili kufikisha ujumbe kwa wengine na hatimaye kila mmoja kufahamu umuhimu wa haki ya kupata habari.

"Ninawaomba mjitahidi kufanyia kazi mafunzo haya na pia myapeleke kwa mwenzenu, mkifanya hivyo mtakuwa mmetimiza jukumu lenu la kuelimisha," Mukajanga alisema.

Mwandishi Mwandamizi na Mkufunzi wa MCT, David Mbulumi, aliwakumbusha waandishi wa habari kupenda kusoma sheria ili kufahamu haki zao na za jamii wanayoihabarisha.

"Tusome sheria, tujifunze sheria, kuna mambo mengi ya kujifunza kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu, hii itatusaidia kufanya kazi kwa weledi zaidi," alisema Mbulumi.

MCT pia imewataka waandishi wa habari wote nchini kupeleka taarifa zinazohusiana na unyanyasaji zilizotokea katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu ili zifanyiwe kazi.

# Kamati zaTPSF zaja kuweka sawa mazingira ya uwekezaji

**Beatrice Moses**

MWENYEKITI wa Bodi ya Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini(TPSF), Angelina Ngalula, amezindua kamati saba za bodi ya TPSF ili zitakazopendekeza uboreshaji wa mazingira ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji nchini.

Kamati zilizozinduliwa ni Kamati ya Programu na Maendeleo ya Biashara, Kamati ya Fedha na Utawala, Kamati ya Ukusanyaji rasilimali endelevu, Kamati ya Uwekezaji, Kamati ya Huduma za Uwanachama, Kamati ya Sera, Tafiti na Ushawishi na Kamati ya Ukaguzi na Tahadhari.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Ngalula amezitaka kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na kuwataka wafanyabiashara kuwa wazalendo, wawajibikaji na wawazi katika ulipaji kodi ili kuiwezesha serikali kufikia malengo yake.

"Serikali ya awamu ya Sita imejiwekea malengo ya kukusanya kiasi cha Sh. trilioni mbili kila mwezi kutokana na kodi hivyo ni nafasi kwa sekta binafsi kuiwezesha serikali kufikia malengo hayo kwa kulipa kodi stahiki na kwa wakati," amesema Ngalula.

Akisema ili kufanikiwa kupata masoko hasa ya nje ya nchi ni lazima kwa kamati hizo ziwe na uhusiano mzuri na kuwatumia wanadiaspora waliopo nje ya nchi.

"Kuna wenzetu wengi tu wapo nje ya nchi. Hawa endapo tutawatumia vyema itakuwa rahisi hata kwetu sisi kuweza kupata masoko ya nje," alieleza Ngalula.

Pia Ngalula alizitaka kamati hizo kuhakikisha zinatafuta namna ya kuwajengea miradi na uwezo vijana ambao amesema ni taifa la kesho.

"Kuna idadi kubwa ya vijana ambao kwa namna moja wanakwama kufikia malengo yao kwa kuwa tu hawajajengewa uwezo wa kujua namna ambavyo wanaweza kunufaika na fursa mbali mbali zilizopo." alisema Ngalula.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sera, Tafiti na Ushawishi ambaye pia ni Mbunge wa Kibaha, Sylvestry Koka, alisema kamati itahakikisha changamoto za kisera zinatatuliwa ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa wafanyabiashara katika upangaji wa viwango vya kodi na kutoa ushauri utakaoleta manufaa katika maendeleo ya nchi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Utawala, Mercy Silla, amesema ili kuwepo na maendeleo endelevu ya ndani na taasisi ni muhimu kuhakikisha suala la utawala, uwazi na usimamizi wa fedha linasimamiwa kwa umakini na uzalendo mkubwa ili kujenga imani kwa wanachama juu ya mapato na matumizi na hali ya utawala kwa ujumla.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Francis Nanai, amesema sekretarieti imejipanga vyema kuhakikisha mipango na malengo waliyojiwekea yanafanikiwa huku akikiri kuwa suala la kutengeneza uhusiano na wanadiaspora linatija kubwa kwa ustawi wa wafanyabiashara nchini.

## JKT yaja na mwarobaini wa sumu kuvu

**Na Renatha Msungu,** SONGEA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), linatarajia kujenga maghala ya kuhifadhi vyakula katika kambi za Jeshi ili kuepukana na wadudu wanaosababisha sumu kuvu katika mazao ya chakula.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa ziara katika kikosi cha 842 JKT Mlale kilichopo Songea mkoani Ruvuma, ya kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kilimo Mkakati (2020/21-2024/25), Mkurugenzi wa Idara ya Kilimo ya Jeshi hilo ambaye pia ni Katibu wa Kamati ya Kilimo mkakati, Luteni Kanali Peter Lushika, alisema moja ya mkakati waliojiwekea ni kulima mazao ya kutosha ili kukidhi mahitaji ya chakula jeshini na nje ya jeshi.

Alisema maghala yanatarajia kujengwa na kwamba mengine ambayo tayari yamejengwa yatakuwa na uwezo wa kuhifadhi magunia mengi ya mazao ya chakula kuanzia magunia 80,000 -100,000 kwa ghala moja.

Alisema uhifadhi mzuri wa mazao hayo utasaidia pia kupunguza tatizo la sumu kuvu nchini kama siyo kulimaliza kabisa.

Luteni Kanali Lushika alisema ujenzi wa maghala hautaondoa tu upotevu wa chakula lakini pia utaondoa tatizo la sumu kuvu ambalo linaleta madhara makubwa kwa walaji.

"Mpango huu umejikita pia katika uhifadhi wa chakula, lengo ni kuhakikisha mazao yanahifadhiwa vizuri… wataalamu wanasema asilimia 60 ya mazao yanaweza kupotea kama hakuna uhifadhi mzuri," alisema Luteni Kanali Lushika.

Alifafanua kwamba Jeshi hilo linaendelea na ujenzi wa maghala ambayo yatawezesha kuhifadhi mazao wanayolima, na kuwa pia watahifadhi mazao ya wananchi ili yawe salama kwa matumizi ya binadamu.

Aliongeza kuwa ujenzi wa maghala unakwenda sambamba na uzalishaji wa mazao ya kilimo, mpaka sasa JKT lina maghala katika vikosi vya Milundikwa kilichopo Sumbawanga ambacho kina uwezo wa kuhifadhi magunia ya mahindi 80,000 hadi 100,000 na Chita mkoani Morogoro lenye uwezo wa kuhifadhi magunia ya mpunga 40,000.

Hata hivyo alisema,kutokana na uzalishaji mkubwa wa zao la mpunga unaofanywa katika kikosi hicho, JKT inajenga ghala kubwa zaidi .

# Msako sasa kiwanda hadi kiwanda

SERIKALI imeanza kuvipitia viwanda vyote ambavyo havifanyi kazi hasa vilivyobinafsishwa kwa watu na hawaviendelezi ili kuvifufua, Bunge lilielezwa jana mjini hapa.

Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017/18 mpaka 2019/20, wanafunzi 228 walihitimu shahada ya sayansi katika Menejimenti ya Uhandisi wa Viwanda 228, huku kati yao 55 walipata ajira.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu maswali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christine Mnzava.Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kuongeza viwanda vingi ili wanafunzi wanapohitimu wapate ajira kutokana na vijana saba tu ndio walioajiriwa na serikali.

"Nini mpango wa serikali kufufua viwanda vyote ambavyo vilijengwa enzi za Mwalimu Nyerere ili hawa vijana wetu wapate ajira?" alihoji.

Pia alihoji serikali inawatumia vipi wanafunzi wanaohitimu shahada hiyo katika uchumi wa kati wa viwanda.

"Je, ni wanafunzi wangapi waliohitimu katika fani hiyo wameajiriwa serikalini tangu mwaka 2019 hadi 2020?" aliuliza.

Akijibu maswali hayo, Kigahe alisema serikali inavipitia viwanda hivyo ili kuvifufua.

"Lengo ni kuona sekta ya viwanda inaendelea kwa kutumia miundombinu ya viwanda iliyokuwapo kabla ili wataalamu wanaosoma kwenye vyuo vyetu waajiriwe kwenye viwanda hivyo," alisema.

Kuhusu ajira, Naibu Waziri huyo alisema kati ya wahitimu hao 55 waliopata ajira, saba pekee ndio waliajiriwa serikalini.

Alifafanua kuwa shahada hiyo ilianzishwa mwaka 2015 katika Chuo Kikuu cha Mzumbe ikilenga kuzalisha wataalam wa kusimamia shughuli za uzalishaji katika viwanda ambavyo vinamilikiwa na serikali na vile vya mashirika au kampuni binafsi.

"Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017/18 mpaka 2019/20, wahitimu wengi wa fani hiyo wameajiriwa katika sekta binafsi hususan katika viwanda vya kuzalisha bidhaa kama vile saruji, vinywaji, nguo, sukari, vyakula, mbao, vifungashio, mafuta na uchimbaji wa madini," alisema.

Pia alisema wahitimu hao wameajiriwa katika taasisi za serikali zinazoshughulikia masuala ya ubora ikiwamo Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Taasisi zingine ni Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda (TIRDO), Chuo Kikuu cha Mzumbe, Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Hata hivyo, alisema kwa kuwa serikali inatekeleza azma ya ujenzi uchumi wa viwanda, wahitimu katika fani hiyo walioajiriwa wanatumika katika usimamizi wa shughuli mbalimbali za viwanda vilivyoko katika sekta ya umma na binafsi.

Kigahe alisema mpango wa serikali ni kuhakikisha kunakuwapo na viwanda vingi kwa kuhamasisha sekta binafsi kwa kuweka mazingira wezeshi ili wawekezaji wajenge viwanda vingi vitakavyotoa ajira kwa vijana hao.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (kushoto), Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi (wa pili kushoto) na Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Mbunge aibana serikali kuhusu ahadi barabara

MBUNGE wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, ameiomba serikali kutimiza ahadi yake ya ujenzi wa kilomita tano za barabara kwa kiwango cha lami katika mji wa Ikungi mkoani Singida.

Akiuliza swali hilo bungeni jana, Mtaturu alitaka kujua lini serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo ili kutimiza ahadi iliyowahi kutolewa na Waziri Mkuu mwaka 2019.

"Kwa sababu mji wa Ikungi ni wilaya mpya na kwa sababu makao makuu ya wilaya tunategemea yawe na lami na Waziri Mkuu mwaka 2019 alituhakikishia kujengwa kwa barabara hiyo na leo ni 2021, ni lini sasa fedha zitatengwa?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri,Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali kupita Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imepanga kufanya usanifu na tathmini ya gharama za ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami katika mji wa Ikungi.

Alisema utambuzi wa barabara hizo utakuwa shirikishi ili kutoa kipaumbele kwenye barabara zenye umuhimu mkubwa.

"Hadi Machi 2021, TARURA imetoa Sh. milioni 598.22 kati ya Sh. milioni 890.89 zilizotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 97.92 katika ya Wilaya ya Ikungi," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali itaomba kuidhinishiwa Sh. milioni 925.08 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 92.6.

Aidha alisema Sh. bilioni 1.4 zitatengwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Mihyuge wilayani Ikungi.

Silinde alisisitiza kuwa serikali itaendelea kufanya usanifu na kujenga barabara kwa kiwango cha lami kwenye maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo Ikungi, kulingana na upatikanaji wa fedha.

## Mradi ujenzi VETA Ludewa kuendelea

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi (VETA) Shaurimoyo wilayani Ludewa, utaendelea kupitia Mradi wa Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi (ESPJ ) na utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.3.

Naibu Waziri, Omar Kipanga, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ludewa (CCM), Joseph Kamonga.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itakamilisha ujenzi wa chuo hicho ili kuzalisha wataalam watakaosaidia kutekeleza mradi wa Liganga na Mchuchuma utakapoanza.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kipanga alisema mradi huo utatekelezwa kwa utaratibu wa 'force account'.

"Tathmini ya gharama imeshafanyika ambapo jumla ya Sh. bilioni 4.342 zitatumika kukamilisha ujenzi huu," alisema.

Alifafanua kuwa ujenzi wa chuo cha ufundi stadi na huduma cha Mkoa wa Njombe, kinachojengwa katika wilaya ya Ludewa ni miongoni mwa vyuo vilivyokuwa vinajengwa na wizara kupitia mradi wa kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya ualimu (STVETTE).

"Mradi huu ulikuwa unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mkataba kati ya serikali na benki hiyo uliisha muda wake Desemba 31, 2019 kabla mradi haujakamilika," alisema.

Alisema kutokana na umuhimu wa kukamilika kwa mradi huo, utekelezaji wa mradi huo utaendelea kupitia Mradi wa ESPJ.

Kipanga alibainisha kuwa ujenzi wa chuo hicho unatarajiwa kuanza tena katika Mwaka wa fedha 2020/21.



ama
ALHAMISI APRILI 22, 2021
AFYA NA MAZINGIRA







# Mkurugenzi Kinga: Ukihisi ujauzito, mara moja anza mchakato huu hapa

• Dk. Maro, ataja vigingi utakavyovikuta

**Na Maulid Mmbaga**

KUNA kinamama wanapopata ujauzito, wanakuwa na swali katika nafsi kuwa, ni lini hasa anapaswa kuanza kuhudhuria kliniki ya afya ya uzazi? Baadhi katika kundi hilo wanajikuta wanachelewa kuanza huduma hiyo.

Wapo wanaoshauri muda mwafaka wa kuanza kliniki ya afya ya uzazi kwa mama mjamzito, ni pale anapogundua hali hiyo, pia inashauriwa mwanamke anakuwa amepanga mwezi wake na wanaanza kliniki mara moja.

Kitaalamu inaelezwa, kliniki ya afya ya uzazi haishii kwa mama pekee, bali kinabana nao wanahusika, wakiandamana wenza.

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk Leonard Subi, anawataka kinamama kuwahi kliniki mara wanapohisi ujauzito kufuata ushauri wa wataalamu wa afya, ili kujilinda, pia mtoto mtarajiwa, kupitia miongozo ya afya.

Dk. Subi anaeleza utafiti uliofanywa mwaka 2010, maambukizi ya virus yalikuwa asilimia 26 kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, huku uliofanywa mwaka 2016/2017 unaonyesha maambukizi hayo yamepungua kufika asilimia 7.6 na matarajio ya sasa mwaka 2020/21, ni kwamba yatapungua hadi asilimia mbili.



Mkurugenzi wa Huduma za Kinga katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk Leonard Subi. **PICHA: MTANDAO.**

“Ni muhimu kwa wajawazito kuhudhuria kliniki na kupima (VVU) hii itasaidia kuzuia maambukizi hayo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

“Malezi na makuzi mazuri ya mtoto yanategemea wazazi wote wawili, yaani baba na mama, wazazi wote wanapaswa kushirikiana hasa katika kupima afya, ili mtoto atakayezaliwa asiwe na maambukizi,” anasema.

Kwa mujibu wa Dk. Subi, kikwazo kimojawapo kinachokwamisha mpango huo, ni baadhi ya wanaume kukumbatia tabia ya kutoandamana na wenza wao kliniki katika kipindi cha ujauzito.

Daktari huyo anaweka angalizo kwamba, ni vyema familia au makabila yanayokumbatia imani mwenendo wa baba kumsindikiza mwenza wake kliniki ni kujishushia hadhi, waachane nazo.

Ujumbe wa aina hiyo, pia anawapatia vijana wanaopaswa kuchukua hatua kwenda katika vituo vya afya kupatiwa elimu ya uzazi na kupima afya zao, kwa maana wao ndio ‘mama na baba’ watarajiwa.

Mkuu huyo wa Kinga serikalini, anakumbusha hatari zitokanazo na mimba za ututoni dhidi ya afya zao, kwani wenye matatizo wanapaswa kufika katika vituo vya afya, kupata msaada wa kitalaamu.

Dk, Subi ana msisitizo kwa vituo vya kutoa huduma za afya vyote nchini, hivi sasa huduma ya elimu hiyo inapatikana bure na hata mjamzito atakapogundulika kuwa na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), ataanzishiwa dawa za kinga mara, ambazo ni za bure.

“Ni jukumu la wataalamu wa afya kuwahudumia wanawake na watoto bila kikwazo, ikiwa ni njia mojawapo ya kupunguza na kuondoa kabisa vifo vya akina mama na watoto nchini,” anasema.

“Naagiza waganga wakuu wote nchini kununua na kuweka televisheni katika vituo vya afya na hospitali ili kuwapatia fursa kinamama kujifunza afya ya uzazi ikiwa ni njia ya kupunguza vifo vya kina mama wajawazito,” anasema.

Anasisitiza wajawazito kujali afya zao kwa kuhudhuria kliniki kwa wakati, ili wapate huduma sahihi, ikiwa na manufaa ya kulinda afya zao, pia watoto waliopo tumboni.

**MCHANGO WA MJAMZITO**

Mganga Mkuu wa Kituo cha Afya cha TMH, cha jijini Dar es Salaam, Dk. Isack Maro, anakumbusha umuhimu wa mama mjamzito kuhudhuria kliniki, ili kujua maendeleo ya ukuaji wa ujauzito na kupata maelezo muhimu kutoka kwa wataalamu wa afya.

“Hakuna kitu muhimu kama kwenda kliniki kwa mama mjamzito na hili tunalisisitiza miaka yote. Changamoto kubwa inayotokea kwetu sisi kwa wengi wanaopata matatizo, huwa wanakuwa walichelewa kuanza kliniki na kutokuzingatia elimu inayotolewa,” anasema.

Pia, anaeleza kuwa kuna baadhi ya maeneo ambayo wajawazito hujifungulia nyumbani, jambo analolitaja si salama na hatari kwa mama na hata mtoto anayezaliwa.

“Kuna mambo yanayoweza kumfanya mtoto asiweze kutoka kama mtoto akiwa mkubwa na nyonga ikiwa ndogo, itasababisha mtoto kukwama njiani,” anasema.

Anataja lingine ni kwamba, mtoto anaweza kukaa vibaya, mathalan kichwa kiko tofauti na kinavyotakiwa kuwa, pia itasababisha ashindwe kutoka.

Katika hila anasema, kuna mazingira utaratibu wa mama kuweza kumtoa unaweza ukafanikishwa, lakini ua muhimu kama vile kitovu kujiachia, inaweza kusababisha madhara kwa mama, pia mtoto.

“Jambo muhimu ni kwenda kliniki na kuzingatia maagizo yote atakayopewa na wataalamu wa afya na kuhakikisha kwamba atakapohisi uchungu aharakishe kwenda hospitali,” anahitimisha kwa msisitizo.

MAZINGIRA

## MJUMITA YATAMBA USHINDI...

# Hifadhi shirikishi inavyoviamsha vijiji kutoka janga la kuteketeza mazingira

**Na BeatricePhilemon, aliyekuwa KILINDI**

MTU anapozungumzia uhifadhi wa misitu na usimamizi wake shirikishi, inaweza kuwa msamiati mgumu kwa sababu wapo wasiolewa vizuri.

Hilo linapoelekezwa katika uhalisia ndani ya misitu ya wilayani Kilindi mkoani Tanga, ambako Nipashe ilizuru hivi karibuni, kuna mlolongo wa faida zinazojumuisha uhifadhi vijiji humo.

Baada ya kuonekana walakini huo, Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) umeanzisha kampeni ya kufundisha wananchi kuhusu usimamizi shirikishi wa misitu, utawala bora na fedha, ili kufikia usimamizi shirikishi wa misitu yao.

Lingine linahusu haja ya kuwapo uwazi katika matumizi ya fedha zitokanazo na mazao misitu na kufuata utawala wa sheria, kwa sababu msitu una usimamizi wake unaoendana na taratibu, kanuni na sheria.

Kimsingi, ni mustakabali unaojumuisha usimamizi, uvunaji mbao na magogo, unaofanywa kwa kushirikisha wananchi kupitia Mkutano Mkuu wa Kijiji chao.



Watumbuizaji wa Kabuku Sanaa Group, wakifanya maigizo kuelimisha jamii kuhusu usimamizi shirikishi wa misitu kijijini Mnkonde, wilaya ya Kilindi. **PICHA ZOTE : BEATRICE PHILEMON**.

### UJUMBE UNAFIKISHWAJE?

Ili kuwapo hali shirikishi ya umma husika, kama vile wanakijiji, asasi ya Mtandao wa Jamii na Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), imeamua kufanya ubunifu.

Hapo kunatajwa kutumia ngoma za asili, maigizo, ngonjera, muziki kuwahamasisha, huku kukitumika video kuwaonyesha wananchi wanachokifanya wenzao katika vijiji vingine kuhifadhi misitu na faida wanazopata na namna wanavyowajibika.

Mratibu Msaidizi wa MJUMITA Kanda ya Kaskazini, Hamisi Masinde, anaiambia Nipashe kwamba, wameshaanza kutoa mafunzo kwa kutumia myenzo kadhaa kama vile ngoma za asili, maigizo, ngonjera, video na muziki katika vijiji vya Mnkonde na Bandari Mkomazi, wilayani Kilindi.

"Kwa kutumia njia hii, wananchi wengi wanaburudika na wakati huo huo wanapata ujumbe," anasema.

Mbali na hilo, njia hii inajumuisha watu wa rika zote kwa maana ya watoto, kinamama, baba, vijana na wazee," anasema," anasema Masinde, huku akitaja manufaa ya moja kwa moja ni mageuzi ya kijiji kujua wajibu wake katika usimamizi wa misitu wake.

Ni mafunzo yanayojumuisha utawala bora na usimamizi wa fedha zitokakanazo na mazao ya misitu kijijini, mkufunzi mkuu akiwa Mradi wa Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC), unaofadhiliwa na serikali nchini na wabia wao wa Finland.

"Tumeamua kutumia mbinu hii baada ya kuona asilimia kubwa ya wananchi katika vijiji ambayo tunatekeleza mradi katika wilaya ya Kilindi na Handeni mkoa wa Tanga, hawajitokezi kwenye mkutano mkuu wa vijiji ambao unaitishwa na viongozi wa vijiji," anaeleza Masinde.

Mratibu huyo anakiri bado wananchi wengi hawajafahamu umuhimu wa usimamizi shirikishi wa misitu katika vijiji vyao, jinsi ya kuihifadhi na kusimamia.

Pia, ni aina ya mageuzi katika mfumo wa mafunzi kuwafikia wakazi wote wa kijiji, tofauti na awali mafunzo yaliishia kwa viongozi wa vijiji na kamati ya maliasili pekee inayomjumuisha Mwenyekiti, Mtendaji na Halmashauri ya kijiji.

Kwa mujibu wa Masinde, mradi wa FORVAC unapitia vijiji vitano, ambavyo ni Gole, Mazingira, Kitumbi, Mnkonde na Bandarikomnazi, katika wilaya za Handeni na Kilindi.

### USHUHUDA WA MAGEUZI

Tayari kuna kigezo cha mageuzi, kijiji cha Bandarikomnazi, kilivyoelimika na mafunzo na tayari kimeshaanzisha Mpango wa Usimamizi wa Misitu yake, inayoendana na sheria zake ndogo za kusimamia msitu, kukiwa kumetengwa hifadhi ya kijiji yenye hekta 404.7.

Mweka Hazina wa Kamati ya Maliasili katika kijiji cha Mnkonde, Sophia Masingia, anaiambia Nipashe, kuwa darasa walilolipata kutoka mtandao wa MJUMITA limewaletea mabadiliko wakijua kusimamia msitu wa hifadhi ya kijiji na hadi sasa wamefikia hatua ya mavuno.

"Ingawa tumefikia hatua hii, bado kuna changamoto ya wafugaji katika msitu wetu wa hifadhi ya kijiji, wafugaji wanaingiza mifugo ndani ya msitu, wanalima shamba hata kujenga nyumba za kuishi vitu vinavyochangia uharibifu msitu," anasema.

Sophia anaelekeza ombi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, iwasaidie kuwondoa wavamizi hao wanaodaiwa kutumia mabavu kuishi ndani ya msitu walikokatazwa.

Anasema mradi FORVAC umeshawapa pikipiki ya kufanyia doria msituni na hadi sasa inatumiwa na Ofisa Mtendaji wa Kijiji, huku akitoa rai ya uwezekano wa kupatikana pikipiki kwa ajili ya Kamati ya Maliasili ya Kijiji.

Pia, anaomba wadau waliopo katika sekta ya misitu ikiwamo MJUMITA na Kikundi cha Uhifadhi wa Mazingira Tanzania (TCFG), iwasaidie kupata pikipiki nyingine, mabuti, miamvuli na simu za kazi.

Mengine ni mabango nane ya kuwekwa msituni, kuwasilisha tahadhari na angalizo kuhusu msitu, ikiwamo zuio lake kisheria.

### OFISA MISITU

Ofisa Misitu Wilaya ya Kilindi, Rawland Lema, anasema uhifadhi na usimamizi shirikishi wa misitu ulianza mwaka 2008, akifafanua: "Kabla ya mafunzo uharibifu wa misitu, ulikuwa mkubwa sana katika misitu ya vijiji vyote, ikiwamo kijiji cha Mnkonde, Bandarikomnazi.

"Lakini, baada ya kupata mafunzo na kushirikisha jamii kwa kujengea uelewa juu ya rasilimali misitu zilizopo katika maeneo yao, uharibifu ulianza kupungua kwa kasi.

"Tuliwafundisha kuwa hii ni mali yao na wao ndiyo watumiaji na wanufaika wa rasilimali hizo. Hivyo basi, wananchi wanatakiwa kuhifadhi na kupanga namna ya utumiaji kwa njia endelevu."

Anasema, mamlaka ya wilaya kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, MJUMITA, TFCG na wadau wengineo wamwechukua hatua, akiibebesha simulizi:

"Kwa mfano tumewezesha vijiji vya Bandari komnazi kutenga eneo lenye hekta 404.7 ambazo wamefanya tathimini ya rasilimali zilizopo, ili waweze kuvuna kwa njia endelevu kwa faida ya sasa na vizazi vinanvyoendelea," anafafanua Lema

Mnkonde ni kijiji kilichofanikiwa kutenga hekta 1102 kuwa hifadhi ya msitu wa kijiji uliofikia hatua ya mazao mavuno na kuuzwa, kukiwapo matarajio ya kupata Sh. milioni 290 kwa mwaka.

"Wananchi tunatakiwa kulinda na kusimamia msitu wetu na kuvuna kwa njia endelevu na hapa tupo kwenye hatua ya mwisho na baada ya muda mfupi tutaanza kuvuna msitu wetu," anasema.

Pia katika kipindi hiki cha mvua zinazonyesha mwezi April, wananchi wa kijiji cha Mnkonde wanatarajia kupanda miche ya miti 6000 katika maeneo yaliyowazi ndani ya msitu wa Hifadhi ya kijiji Mbwego na kuzunguka msitu

"Ingawa tunasaidia kuhamasisha jamii kutenga na kuhifadhi maeneo ya misitu , bado sisi kama maofisa misitu hatuna vitendea kazi ikiwamo usafiri, mafuta, fedha na mafunzo juu ya Usimamizi wa misitu," anasema Lema.

"Tunaomba mafunzo kwani tangu tumalize mafunzo mwaka 2010 hadi sasa hatujawahi kupata mafunzo au semina aina yoyote," anahitimisha.




Moja ya matangazo yanayohusu hifadhi ya misitu katika kijiji cha Mnkonde, wilayani kilindi.

AFYA

## KURUNZI YA SHINYANGA VIJIJINI...

# Migogoro familia yaziita kwa kasi VVU na madhara kwa mabinti zao

## •Wametekwa na mila, wachimba madini
## •Ashitakiye kadhalilishwa ni adui wa kijiji

**Na Shaban Njia, SHINYANGA**

UKATILI wa kijinsia si msamiati mpya ndani ya Halmashauri ya Shinyanga Vijijini. Hapo kuna ukweli pia kukosekana elimu ya ukatili wa kijinsia, dhidi ya wanawake.

Ni hali inayosababisha kinamama wengi kuendelea kuwa wahanga wa ukatili, kwa sababn tu wanahofia kuvunja ndoa zao, pia kutengwa na jamii inayowazunguka.

Mwakitolyo ni kati ya kata 26 zinazounda halmashauri hiyo, ikiwa na wakazi 15,000 kwa mujibu wa Sensa ya Makazi ya Mwaka 2012, ikiundwa na vijiji sita: Mwakitolyo, Nyaligongo, Mawemilu, Mwasenge, Nyango'ombe na Mahambe.

Uhalisia ni kwamba, kinamama hao walishakata tamaa ya kupambana dhidi ya ukatili kwao na watoto, ambao tafsiri ya wazi imo katika afya zao.

Ushuhuda wa Nipashe imeambiwa, kila wanapothubutu kutoa taarifa za ukatili husika kwenye madawati ya jinsia, wanatishiwa kutengwa na familia zao, hivyo wanaamua kutotoa taarifa na kuendelea kunyanyasika.

Kuna madai ya baadhi ya wanawake wanaofanyiwa mabaya ya kingono, wanapojaribu kufikisha malalamiko yao katika serikali za mitaa, juhudi zao za kulalamika huishia kukosa msaada wowote.

Ni ushuhuda unaotajwa kuenadana na kutengwa na familia zao, kwa wanawake hao wanashindwa kugharamia safari za kwenda katika Kituo cha Polisi.

Nipashe imeelezwa kwamba, safari ya kufika ilipo dawati la jinsia katika kata jirani ya Salawe, ni umbali kilomita 30, unahitaji nauli ya gari Sh. Sh. 5,000 na pikipiki ni kati ya Sh.15, 000 hadi Sh.20, 000.

Hapo ndipo Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Shinyanga (SPC) kimepewa jukumu hilo la kusaidia kukabili ukatili kwa wanawake na watoto wanaotekelezwa katika Halmashauri ya Shinyanga Vijijini, katika eneo hilo lenye ongezeko wa wakazi asilimia 2.1 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012.

**WAKAZI WANAVYOFUNGUKA**

Veronica Sostenes, mkazi wa Kata ya Mwakitolyo katika Halmashauri ya Shinyanga Vijijini, anasema migogoro ya kifamilia, ndoa za umri mdogo na mimba za utotoni zinachangia kusababisha wasichana wadogo kuendelea kukosa masomo.

Pia, anasema zinachangia kusababisha vifo vitokanavyo na uzazi, maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na saratani ya shingo ya mlango wa kizazi kwa mabinti.

Veronica anasema, ukatili dhidi yao kinamama na watoto wao vinashamiri mahali hapo, hali inayosababisha mabinti kuendelea kukosa masomo, kwa sababu ya migogoro ya familia zao, ndoa na mimba za utotoni.



Wanakijiji wa Mwakityolo, Shinyanga wakiwa katika mkutano wao. **PICHA: MTANDAO**.



Neema Tabu, mkazi wa Kata ya Mwakitolyo, katika Halmashauri ya Shinyanga Vijijini, akimweleza mwanahabari yanayowasibu. Aliyekaa jirani yake ni mwanakijiji mwenzake. **MPIGAPICHA WETU**

Mkazi mwingine wa Mwakitolyo, Godfrey Bahati, anasema jamii zinaendelea kukumbatia mila na utamaduni potofu, unaochangia kuongezeka matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Anatahadharisha kwamba, ni hali ambayo isipochukuliwa hatua za haraka, ina hatari ya kumkwamisha mwanamke kutimiza ndoto zake kielimu na uchumi.

"Vijijini bado kuna wazee wenye umri mkubwa wanaoa watoto chini ya umri wa miaka 18, huku baadhi ya wazazi wakitajwa kushiriki kuozesha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, kwa ajili ya kupatiwa fedha au mifugo bila ya kujua athari zinazoweza kuwapata pindi wanapoolewa," anasema.

Bahati ana angalizo kwamba, ni ndoa hizo zinazoweza kuwa kichocheo cha watoto kupata maambukizi ya magonjwa ya ngono, kutokana na ukweli wengi wao hawana ulewa kuhusu mustakabali wa afya ya uzazi.

Pia anataja kuwapo ramli chonganishi vijijini ambapo waganga wanawashawishi wanaume kufanya mapenzi na watoto wenye umri mdogo, lengo ni kupata mali, madhara yake yakiishia katika mimba na kuambukizwa magonjwa ya ngono.

**KUKOSA KITUO POLISI TATIZO**

Maria Simon, anasema kukosekana kituo cha polisi wangekitumia kuelekeza malalamiko yao katika dawati la jinsia nako kumechangia kuibuka ukatili mpya, wanaume wanatelekeza familia zao, nyuma watoto nao wanakatisha masomo, wakielekea kufanya kazi kwenye machimbo ya dhahabu.

Inadaiwa, pale wanapopeleka malalamiko yao kwa wenyeviti wa serikali za mitaa, huaswa wayamalize ili wasitengwe na familia zao.

"Sio kwamba hatufanyiwi vitendo vya kikatili, tunafanyiwa, lakini hatuna mahali pa kusemea. Wanaotufanyia ukatili," anasema Samweli na kuongeza:

"Hawamuogopi Mwenyekiti wa Kijiji na ukichukua uamuzi wa kuelekea Polisi Salawe, familia inakutenga kwa kumshtaki mumeo au jirani.

Katibu wa Viwanda vya Uchenjuaji Madini Mwakitolyo, Matemla Michael, anasema wana mchango wao katika kupinga ukatili kwa watoto wadogo kujihusisha na uchimbaji madini, upasuaji mawe na kuchota maji.

Anasema, hadi sasa wamechangishana Sh.300,000 za kujenga kituo cha polisi kila mmiliki wa kiwanda cha kuchenjua madini, lengo lililoko ni pindi itakapomilika mkakati utahamia kujenga mahakama, ili kulinda mali zao na kudhibiti ukatili wa kinamama na watoto.

**OFISA MAENDELEO JAMII**

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Kata ya Mwakitolyo, Mussa Gongo, anasema anashirikiana na wenyeviti wa serikali za mitaa na kamati washirika katika kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto, kuhakikisha wenye umri wa shule wakasome.

Gongo anawataka wazazi na walezi kupiga vita vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake, kuhakikisha wanapata haki zao za msingi ikiwamo elimu na kutengeneza taifa lenye wasomi.

Anasema kuwa, kila siku anapokea kesi zaidi ya sita za wanawake kuachwa na kunyimwa matumizi na waume zao, sehemu kubwa ni kutoka vijiji vya Mwakitolyo na Nyaligogo, huku akihitimisha: "Haiwezi kupita siku mbili, kesi za ukatili wa kijinsia hazijaripotiwa."

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwakitolyo, Samson Lutonja, anawataka kinamama hao watoe taarifa za ukatili dhidi yao, ili wapatiwe ufumbuzi wa haraka, kuwezesha watoto wasome na kutimiza malengo yao, sio kufanya kazi migodini.

Anasema amekuwa akishirikiana na wadau wengine kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwenye mitaa yote ya Mwakitolyo kupitia mikutano ya hadhara, lakini anaeleza wananchi kushangazwa pale wahudhuriaji wanapogundua hakuna ajenda ya kuchimba madini, wanaondoka.

AFYA

# Mazingira yenye kitendawili mabinti kuanzisha familia katika utandawazi

**Na Michael Eneza**

SIKU ya Kimataifa ya Wanawake mwezi uliopita, imewezesha mwendelezo wa mijadala katika maeneo kadhaa yanayogusa mikakati ya jumla, inayohusiana na usawa wa kijinsia au mustakabali wa mikakati ya jinsia nchini.

Moja ya maeneo yanayoleta shaka katika mijadala, ni uhaba wa kuoanisha kinachozungumziwa katika jamii katika upande mmoja na kinachojadiliwa katika majukwaa rasmi na upande mwingine.

Kinachozungumziwa sasa katika vyombo vya habari, kinalenga zaidi tabu zinazokumba familia na malezi sasa na lawama inatupiwa mitandao ya jamii, ambayo sasa ndiyo dirisha la kuwasiliana na wengine katika zama zilizopo za 'ubepari mpevu.'

Hiyo, imechukua nafasi katika maongezi na hata hisia ya kinadharia, ambayo kwanza ilikuwa imeshikwa na dhana ya 'ubeberu,' halafu ukabadilika kuwa 'utandawazi.'

Bado dhana za awali zinasikika, ila vianzio vyake ni vichache zaidi, kwani mifungamano ya kimataifa ya kihistoria inayoanzia katika dhana hizo kimsingi imesambaratika.

Kiuchumi na hata siasa ya uchumi, ubeberu uliishia pale kulipovunjika Ukuta wa Berlin, Ujerumani mwaka 1989 na kwa dunia yote ikaanza kuelekea uchumi wa soko na demokrasia, utandawazi ukawa uhuru.

Mitandao inakuwa chanzo cha hisia duni kuhusu utandawazi, kwani kuwapo njia za mawasiliano ni maeneo ya kukutana ya makundi hasa ya vijana kupandikiza hisia mbovu na mwelekeo wa inayochota akili.

Kabla ya hapo, mianya ya kuvutwa kwa hisia za vijana ilikuwapo, kwa mfano fasheni za muziki au mavazi, lakini hapakuwapo mawasiliano ya moja kwa moja kama nyakati za mitandao.

Wakati simu za 'kiganjani' zinaingia mwaka 1994 zilikuwa hasa zinamilikiwa na mamilionea, 'utandawazi' ukahakikisha kuwa kila anayetaka anakuwa na simu 'janja' wakati wowote.



Wanafunzi wasichana wakiwa katika hadhira inayowahusu. **PICHA: MTANDAO**

**SAFARI YA UZAZI**

Ndiyo hapo inazaliwa dhoruba ya mwelekeo wa uzazi na malezi katika karne iliyopo hata katika nchi za Afrika, kwani kusambaa sekondari huru nchini kunaanza kuondoa hali ya uwapo 'dada wa kazi' katika nyumba nyingi.

Kabla ya kuenezwa zaidi shule za sekondari za kata, ajira ya watoto waliomaliza shule ya msingi, au hata bila kumaliza ngazi hiyo, ilikuwa inapigwa vita katika mkakati wa jumla wa kuwalinda wanawake na watoto, dhidi ya kutumikishwa au ndoa za utotoni.

Uwapo wa shule za sekondari bure katika kile kilichowavutia zulia, ambako utumikishaji ulijishikiza, kuna suala la kukosekana vijana wa kile kinachosaidia kazi nyumbani, hali inayosaidia mikakati ya kifamilia ya kinamama wenye elimu na wanaounda familia.

Vivyo hivyo, kuna wanaofanya kazi wakati ambao sekondari hizo pia zinaweka mstari wa kuzuia nani anaweza kuolewa.

Hiyo ina maana kuwa, mustakabali wa kufikia lengo la kinamama '50 kwa 50' chenye chanzo cha mkutano wa Beijing, utaanza kushika kasi, kwani vijana wana kile wakishavuka kizuizi cha sekondari, inakuwa rahisi zaidi kuweka akili zao katika malengo ya kitaaluma kuliko kuolewa.

Matokeo yake ni kuwa hii hali ya kutokuwapo wasichana wa kazi za ndani, hatimaye itajitokeza suala la kuolewa kwa waliomaliza sekondari na vyuo, kwani hawakubali mtu yeyote tu na kwa jumla, hawana imani na wengi wanaowataka.

Siyo rahisi kutamka, suala la kutoendelea na sekondari kwa wasichana wengi, kuliwezesha kwa kiasi gani kuundwa familia za vijana wanaume wenye mazingira ambayo yana uhitaji ndani yake.

Kuendelea na sekondari kunamvusha msichana katika kipindi cha hatari ambacho mawazo yake yanatawaliwa na watu wengine, kwa mfano wazazi kuambiwa kuna mtu anataka kumuoa na kumfikisha katika ngazi ya kujiamini zaidi.

Anapofika hali hiyo, anakuwa na uwezo angalau wa kushiriki kwa mbali katika mkakati wa '50 kwa 50', yaani kuwa na malengo binafsi ya mafanikio katika maisha, si utii wa kinyumba.

Hata yanapofikiwa mazingira ya kuanzisha familia au kukubali pendekezo la kuanzisha familia, kuna athari za malengo ya '50 kwa 50' kwa mwanamke anapokuwa katika mkakati binafsi wa mafanikio.

Mara zote haendeshi maisha kulingana na mazingira ya kifamilia atakayoyakuta, ila anaamua kama anakubali kuishi katika mazingira kama hayo, au aendelee 'kivyake' akiwa hana dada wa kazi, atapangaje uzazi, malezi?

Mazingira yanayowezesha kuwa na matazamo ya kuendelea kuwapo urahisi kiasi fulani kwa vijana wanaotaka kuanzisha familia kufanya hivyo, ni uhaba wa nafasi baada ya kufikia elimu ya sekondari.

Sehemu kubwa ya mabinti wanaofikia ngazi hizo watakapokosa uwezo au nafasi za kusomeshwa, wataingia ndani ya hasara hiyo ya 'unyumba haraka zaidi' na wanapobaki mafunzoni wanakuwa hawana bughudha

ya karibu ya mimba.

**SHIDA YA MALEZI**

Siku zote inabaki kuwa shida katika kupanga uzazi na malezi. Endapo mdau wa familia anaingia katika malengo ya '50 kwa 50' ambayo katika maisha ya mijini ni magumu kufanikiwa bila ya kuwa na msaada wa 'dada wa kazi.'

Hapo kuna kikwazo kingine kimeshazaliwa cha kiulizo, atasomaje? Mtu anaweza kudai kuwapo dhana 'mapinduzi ya utamaduni' nchini yanatokana na wimbi la '50 kwa 50', yaani wanaume na wanawake kugawana nafasi katika ngazi takribani zote, isipokuwa kwenda 'leba' hospitalini.

Uhalisia unachukua sura, ni haja ya kutaka mabinti waondolewe katika janga la kutumikishwa baada ya darasa la saba au hata bila kumaliza ngazi hiyo.

Kitendawili kingine kinaangukia mijini, ni namna gani wanawake watakuwa na watoto pasipo kujengewa mazingira sahihi ya kupata familia na wakati huohuo, kun maendeleo mengine.

Majibu sahini yanabeba mahitaji ya mkakati wa '50 kwa 50' unaohitaji kumjumuisha kila msichana na 'sapoti' ya jamii kwa upana wake, ili mtawanyiko wao wa baadaye kielimu ufanane na wanaume.

Ili kuanzisha familia katika umri unaofaa, mwanamke ni stahiki katika kipindi cha kupendeza na hitaji la kutambuliwa,

Fedha nazo ni muhimu kwake, na ujumla wake kuna ugumu wa kumuachia, binti aache kuunda familia kwa mbadala wa kudai fedha kwanza, halafu waamue kuwa na familia. Tayari kunakuwapo kitendawili.



## Shule yasaidiwa ukarabati wa mifumo ya maji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BENKI ya Equit Tanzania imetoa msaada wa Sh. milioni 10, kwa ajili ya kufanya ukarabati wa mifumo ya maji katika Shule ya Msingi Makole jijini Dodoma ili kuondokana na tatizo la upotevu wa maji.

Akikabidhi msaada huo kwa Waziri wa Maji, Juma Aweso, Mkurugenzi mwendeshaji wa benki hiyo, Esther Kitoke, alisema lengo la msaada huo ni kuunga mkono jitihada za serikali kupambana na tatizo la upotevu wa maji.

Alisema, msaada huo utasaidia kufanya matengenezo ya mifumo ya usambazaji maji katika shule ili kukabilina na upotevu wa maji.

"Kiasi hichi cha fedha tumekitoa kama sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kupambana na tatizo la upotevu wa maji unaosababisha kupotea kwa kiasi kikubwa cha mapato ya serikali," alisema Kitoke.

Naye Mkuu wa idara ya biashara wa benki hiyo, Isabela Maganga, alisema kuwa wao kama moja ya wadau katika kampeni ya kudhibiti upotevu wa maji nchini wanao wajibu wa kuhakikisha maji yanayozalishwa yanahifadhiwa vizuri.

Alisema wanashirikiana na mamlaka mbalimbali za maji nchini kupambana na kero ya upotevu wa maji yaliyozalishwa kabla ya kumfikia mteja.

"Pia katika kampeni hii sisi tumeanzisha njia ya kusaidia kuwafikishia wananchi huduma ya maji kwa kuanzisha huduma ya mkopo kwa ajili ya kuunganisha maji ambapo mwananchi anakopa fedha ambazo sisi tunalipa katika mamlaka za maji husika na yeye analipa kwetu kidogo kidogo," alisema Maganga.

Alisema kuwa, kiasi kingi cha maji nchini kimekuwa kikipotea kabla ya kumfikia mteja, kutokana na sababu mbalimbali ukiwamo wizi.

Alisema wananchi wengi bado hawana huduma hiyo ya maji hivyo wengi wao kujiunganisha kinyume cha sheria, hali ambayo inasababisha kiasi kikubwa cha maji kupotea na kuinyima serikali mapato.

"Hivyo basi kupitia elimu pamoja na huduma hii ya mikopo tutahakikisha kuwa watu wengi wanapata huduma ya maji ili kuondoa tatizo hili la upovu wa maji nchini, "alisema Maganga.

Pia, alisema wanatoa elimu kwa wananchi ili wasiharibu miundombinu pamoja na vyanzo vya maji na walipe ankara zao za maji kwa wakati katika mamlaka husika.

"Sisi tupo pamoja katika kampeni hii, tunasaidia wananchi kupata huduma za maji katika maeneo yao na kuondokana na tabia ya wizi wa maji katika mamlaka zetu," alisema

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, alisema kuwa msaada huo ni muhimu na umekuja wakati mwafaka kwani utasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa tatizo la upotevu wa maji katika eneo hilo.

# Kalemani: Marufuku kuuza mafuta yasiyo na vinasaba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amepiga marufuku vituo vya mafuta kuuza mafuta ambayo hayana vinasaba vinavyolenga kudhibiti viwango na ubora wa bidhaa hiyo.

Pia, ametoa siku mbili kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), kuhakikisha wanakagua vinasaba kwenye maghala ya kuhifadhia mafuta.

Dk. Kalemani alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipofanya ziara ya kushtukiza kukagua vinasaba katika baadhi ya vituo vya kuuzia mafuta ikiwamo GP 88 na Total.

Alisema ziara yake hiyo imetokana na kuwapo na taarifa kuwa mafuta yanauzwa bila kuwekewa vinasaba kazi.

"Uwekaji wa vinasaba awali ulikuwa unafanywa na kampuni ya JFI lakini serikali Februari 5, mwaka huu kazi hiyo tuliagiza TBS,na hapa naagiza Makatibu Wakuu wa Wizara za Nishati na i ya Maji kuwafuatilia maofisa wawili wa EWURA ambao wanadaiwa kutotekeleza maagizo ya serikali ya kutaka Februari 5 mwaka huu TBS ianze kazi ya kupima vinasaba," alisema.

Alisema serikali itaendelea kuwekea viwango mafuta yanayouzwa hapa nchini ili kuokoa fedha ambapo kazi hiyo ikifanywa na TBS, Serikali itaokoa Sh. bilioni 3.8 kila mwezi ambazo zilikuwa zinalipwa kwa kampuni hiyo.

Aliongeza: "Sitaki kusikia mahali popote mafuta yanauzwa hayana vinasaba, tutachukua hatua kali sana. Maelekezo yangu nii marufuku kuuza mafuta ambayo hayana vinasaba."

Alisema atatuma mtu afuatilie suala hilo Dar es Salaam na endapo akibaini kuna ghala la mafuta halina vinasaba hatua zitachukuliwa kwa TBS na EWURA.

Alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Joseph Ng'enya, kuhakikisha wanafuatilia kwa kuweka vinasaba kwenye mafuta na kuhakikisha hakuna mafuta yanayouzwa ambayo hayana vinasaba.

Naye, mmiliki wa kituo cha kuuzia mafuta cha GP88, Kessy Halleluya, alisema kampuni imetoa mwongozo kwa madereva wao kutoruhusiwa kutoka kwenye ghala bila mafuta kuwekewa vinasaba na kupewa nyaraka zinazothibitisha hilo.

"Kule depot kuna usimamizi wa EWURA ambao hawaruhusu kutoa mafuta yasiyo na vinasaba," alisema.

Dk. Ng'enya alisema TBS iko tayari kufanya kazi hiyo suala hilo kwa ukaribu.



Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kinyambwa, Kata ya Hazina, jijini Dodoma, Lukanus Kayombo, akizungumza na wakazi wa mtaa huo juzi, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa mabomba ya majitaka ambao unaotarajiwa kugharimu jumla ya sh. milioni 270.5. Kushoto ni Ofisa Maendeleo wa kata hiyo, Mary Shule na Mtendaji wa Mtaa huo, Desderius Bukori. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ummy aombwa kutatua mgogoro Sumbawanga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kwela (CCM), Deus Sangu, amemwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, kushughulikia mgogoro uliopo ndani ya Halmashauri ya Sumbawanga.

Mgogoro huo ni wa kiuhusiano ambapo inadaiwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo amekuwa akiwadharau madiwani na mbunge huyo.

Akichangia jana hotuba ya bajeti ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2021/22, Sangu alisema maendeleo kwa wananchi ni vigumu kuwafikia kutokana na Mkurugenzi kuwa na kiburi na amekuwa akiwatukana viongozi hao.

"Mkurugenzi ana kiburi kama anafikia hatua ya ama amefikia hatua ya kumtukana Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya kuna maisha hapo tena, halmashauri imebaki kama kijiwe tu pale, na juzi mmepeleka Sh. bilioni 2.5 kazifuatilieni fedha hizi za mradi maana kumebaki kama kijiweni,"alisema.

Aidha, alisema: "Mimi sitaki mchezo wananchi wamenichagua, nakuomba sana Waziri tutakutana kwenye shilingi na Halmashauri yangu inaheshimika, hivi kweli unatukana hadi Kamati ya Bunge kwamba nimeteuliwa na Rais mtu anayeweza kunihoji ni Rais tu, hebu tuangalie na Waraka wa mwaka 2011 mmewapa sana mamlaka wakurugenzi na mwishowe wameanza matusi."

Sangu alisema Mkuu wa Mkoa pamoja na Katibu Tawala wa Mkoa wamewasilisha barua nyingi Tamisemi kuhusu suala hilo lakini bado halijapatiwa ufumbuzi.

Kuhusu mgawanyo wa fedha za Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mbunge huyo alishauri uangaliwe mgawanyo wa fedha hizo kama kuna Halmashauri zinapata fedha nyingi.

"Kuna kata hazijawahi kuona hata greda.kuongeze fedha Tarura ni jambo la kwanza lakini la pili wajitahidi mgawanyo unakuwa fair kwa kila Halmashauri," alisema.

Kadhalika, aliomba tarafa ya Kipeta ipate kituo cha afya kwa haraka kutokana na maisha ya wananchi hao kuwa hatarini kwa kufuata huduma ng'ambo ya mto katika kijiji cha Mkulwe.

Pia alishauri mfumo wa ukusanyaji mapato kielektroniki uboreshwe zaidi ili kuepuka kupokea fedha mbichi.

"Katika ripoti ya CAG halmashauri zetu zilikusanya zaidi ya Sh.bilioni 18 hazikwenda benki sababu ya kupokea fedha mbichi, nashauri muende kupitia huu mfumo kwa undani zaidi kwasababu umekuwa na mianya mingi,"alisema.



# Mamia waokolewa biashara haramu

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

WATU 361 wameokolewa kutoka mikononi mwa wafanyabiashara haramu wa kusafirisha binadamu kutoka katika mikoa mitatu ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwenda mikoa mingine na nje ya nchi katika kipindi cha miaka miwili.

Mkurugenzi wa Kituo cha Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu, Ruttagwelela Mutakyahwa, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa mafunzo maalum ya kuwajengea uwezo maofisa maendeleo ya jamii namna ya kudhibiti biashara hiyo.

Alisema watu hao walikuwa wanatoka katika mikoa ya Mbeya, Iringa na Songwe na kwamba kati yao, wanawake asilimia 56 na wanaume ni asilimia 44 huku asilimia 34 ya watu wote ikiwa ni watoto.

Alisema utekelezaji wa udhibiti huo ni maelekezo ya Umoja wa Mataifa ambayo yanataka uzuiaji wa watu hao kutosafirishwa na kwenda kutumikishwa kwenye maeneo waliyokuwa wanapelekwa. "Lakini kuna kundi la vijana wa kiume ambao umri wao unazidi miaka 18 ambao huwa wanachukuliwa kwenda kutumikishwa mashambani, kwenye migodi na kwenye ufugaji, ni kazi zinazohitaji nguvu nyingi," alisema Mutakyahwa.

Alisema pamoja na kufanya kazi ya kuzuia, taasisi hiyo pia imekuwa ikishirikiana na taasisi zingine kuwarejesha Watanzania waliosafirishwa kwenda nje ya nchi ambapo Aprili 15, mwaka huu walipokea Watanzania wanne waliookolewa Mombasa, Kenya wakiwa mbioni kusafirishwa kwenda nchi za Uarabuni kutumikishwa.

Mjumbe wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Kusafirisha Binadamu kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Ahmad Wen-Dadi, alisema biashara hiyo nchini ni kubwa.

Alisema usafirishaji huo wa binadamu ni mkubwa zaidi kwa ndani ya nchi kuliko wale wanaosafirishwa kwenda nje ya nchi na kwamba wengi wa wanaosafirishwa ni wasichana ambao huwa wanaahidiwa kwenda kuajiriwa wanakokwenda.

Alisema wasichana hao wamekuwa wakiahidiwa na wasafirishaji haramu hao kwenda kuajiriwa kwenye maduka makubwa, kazi za ndani na maeneo mengine, lakini wakifika wanakokwenda, wanaishia kutumikishwa kwenye kazi zingine tofauti na matarajio yao.

"Usafirishaji wa nje ya nchi upo pia lakini siyo mkubwa kama huu wa ndani ya nchi, kinachotakiwa kufanyika sasa hivi ni ushirikiano wa jamii nzima kwenye hii vita ya kuzuia biashara hii haramu," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Dk. Jonas Lulandala, aliwataka maofisa hao kujikita katika kuzuia biashara hiyo haramu kwenye jamii kwa kutoa elimu. Alisema kwa takwimu zinavyoonekana, inaonyesha mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inaongoza kwa tatizo hilo nchini, hivyo lazima ushirikiano uwapo ili kulikomesha.

Alisema maofisa maendeleo ya jamii wanaofanya kazi kwenye taasisi za umma na za binafsi, ni kundi muhimu kwenye vita hiyo na hivyo akawashukuru maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Kusafirisha Binadamu kwa kuamua kutoa mafunzo hayo.



Baadhi ya maofisa wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), wakiteketeza dawa za binadamu na mifugo zilizokwisha muda wake katika dampo la Mbalizi, jijini Mbeya juzi, ambazo walizikamata kwenye operesheni waliyoifanya maeneo mbalimbali ya mikoa ya nyanda za juu kusini. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Serikali yaagiza wananchi kulipwa fidia mradi wa maji

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbeya, imeitaka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) kuwalipa fidia wananchi wote waliopisha mradi wa maji wa Mwashali-Isyesye ili mradi huo uwe endelevu.

Vilevile, imeiagiza mamlaka hiyo kuhakikisha mitaa yote inayokizunguka chanzo hicho inakuwa ya kwanza kunufaika na mradi huo ili kuimarisha ulinzi kwa kuwashirikisha wananchi hao. Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alitoa maagizo hayo juzi wakati kamati hiyo ilipofanya ziara kwenye chanzo hicho kwa lengo la kuangalia hali ya ujenzi wake na kuwasikiliza wananchi watakaonufaika na mradi.

Ntinika alisema ili mradi huo uwe na manufaa kwa wananchi, ni lazima mitaa yote iliyokusudiwa kunufaika ipelekewe huduma hiyo haraka na kwamba mradi huo ni miongoni mwa miradi muhimu kwa wakazi wa Kata ya Isyesye ambao kwa muda mrefu walikuwa hawapati huduma.

"Lakini pia tunawaagiza muendelee kushirikiana na wananchi wa maeneo haya kwenye ulinzi wa mradi huu maana mlinzi wa kwanza ni mwananchi ambaye ndiye wa kwanza kunufaika na mradi husika, na niwaambie tu kwamba sisi kama kamati tumeridhika na kazi ambayo mnaifanya," alisema.

Ntinika aliwataka wananchi wa maeneo hayo kuendelea kuvitunza vyanzo vya maji ili viwanufaishe kwa muda mrefu na kwamba hawatakiwi kufanya shughuli zozote za kibinadamu kwenye maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mbeya-WSSA, Edna Mwaigomole, alisema wakati wa ujenzi wa mradi huo wananchi wa mitaa inayozunguka mradi huo walishirikishwa katika hatua zote na kwamba wengi waliajiriwa.

Alisema eneo ambalo wamejenga mradi huo ni lenye mwinuko mkali ambao hauruhusu magari kufika na hivyo waliamua kuwaajiri wananchi kubeba vifaa na kuvipandisha mpaka kwenye eneo la ujenzi. Alisema kutokana na hali hiyo wana uhakika kwamba wananchi hao wataendelea kushirikiana na mamlaka kulinda miundombinu ya mradi huo hata baada ya kukamilika na kuanza kutumika.

"Walifurahi kwanza kwa kuajiriwa na sisi, hili eneo lilikuwa haliwezekani kabisa kufikisha vifaa, sasa tuliamua kuwashirikisha wenyekiti kufanya kazi hii na ndiyo maana mnaona mradi umefikia hatua hii," alisema Mwaigomole.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Kaimu Mkurugenzi wa Mradi huo, Mhandisi Barnabas Konga, alisema miradi yote ambayo mamlaka hiyo imekuwa ikitekeleza inawatumia wataalamu wa ndani badala ya kuwatumia wakandarasi ili kupunguza gharama.

Alisema mfumo huo wa utekelezaji wa miradi unaokoa zaidi ya asilimia 50 ya gharama za utekelezaji kwa maelezo kuwa baadhi ya miradi ikijengwa na mkandarasi huwa wanalazimika kuajiri mkandarasi mshauri, hali ambayo huwa inaongeza gharama.

Konga alisema kuwa kwenye ulinzi wa vyanzo vya maji, wamekuwa wakitumia kampuni binafsi za ulinzi, kamera za ulinzi (CCTV) na kuzungushia uzio kwenye kila mradi.

# NMB yajitosa kero uhaba madawati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHULE ya Msingi Jangurutu iliyoko Kata ya Rujewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, inakabiliwa na uhaba wa madawati, hali ambayo inawafanya wanafunzi kusongamana kwenye madawati machache yaliyopo. Tatizo hilo linadaiwa kusababishwa na shule hiyo kuvuka lengo la uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na awali mwaka huu tofauti na ilivyokuwa inakusudiwa awali.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule hiyo, Oliva George, aliyasema hayo wakati wa hafla ya kupokea zaidi ya madawati 50 yaliyotolewa na Benki ya NMB kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hilo kwenye shule hiyo na Shule ya Sekondari Mengele wilayani humo.

Alisema mwaka huu wameandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza 138 na wa awali zaidi ya 80, hali ambayo imewafanya wavuke lengo na kuzalisha tatizo lingine la uhaba wa madawati.

"Tuna upungufu wa madawati 108, maana mahitaji ya madawati kwa shule yetu ni madawati 251 lakini yaliyopo ni 143 pekee, hali ambayo inawafanya watoto wasongamane kwenye madawati yaliyopo," alisema Oliva.

Akikabidhi madawati hayo kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Straton Chilongola, alisema uboreshaji wa sekta za elimu na afya ndiyo vipaumbele vya benki hiyo.

Meneja huyo alisema sekta hizo mbili ni muhimu kwenye jamii na kwamba ndiyo sababu waliamua kukabidhi madawati kwa shule hiyo ya msingi ili kuisaidia jamii ya watu wa Mbarali.

"Lakini pia tumeamua kuchangia meza 50 na viti 50 kwa shule ya Sekondari Mengele, na hili ni miongoni mwa majukumu ya benki yetu, tunashirikiana na jamii kwenye uboreshaji wa sekta hii muhimu," alisema Chilongola. Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Mfune alikiri kuwapo kwa tatizo la uhaba wa madawati katika shule hiyo pamoja na shule zingine ndani ya wilaya yake huku akiitaka jamii kujitolea kuboresha miundombinu ya shule.





# Dawa za kulevya bado tatizo nchini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud, amesema licha ya juhudi mbalimbali zinazochukuliwa katika kupambana na dawa za kulevya, bado dawa hizo zinaingizwa visiwani Zanzibar.

Aliyasema hayo jana Mazizini, nje kidogo ya Zanzibar, wakati akifungua kongamano la wadau juu ya wajibu wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Masoud alisema ni lazima kuongeza kasi ya kushirikiana katika kupambana na janga hilo ili kufikia kuwa na Zanzibar bila dawa za kulevya.

Alisema kesi za dawa za kulevya zilizoripotiwa polisi ni 654 kwa mwaka 2018, kesi 503 kwa mwaka 2019 na kesi 454 mwaka 2020 na kwamba huo ni ushahidi tosha kuthibitisha kuwa dawa za kulevya zinaingizwa Zanzibar.

Makamu wa Rais alisema ili kufanikiwa katika kupambana dhidi ya janga hilo, ni wajibu wa kila mmoja kutoa mawazo yake juu ya mbinu bora zitakazosaidia kuleta matokeo chanya ikiwamo kuzifanyia kazi kesi za dawa za kulevya zinazochukua muda mrefu bila kumalizika.

"Pia lazima tuhakikishe wahusika wanachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria na kuhakikisha wimbi la uhalifu wa dawa za kulevya linasambaratishwa katika maeneo yote ya nchi yetu," alisema Masoud.

Aidha, alisema iwapo yatasimamiwa hayo kwa uzalendo na kwa uadilifu mkubwa wataiwezesha serikali kujenga uchumi imara na kufikia malengo tuliyojipangia na kupunguza gharama za kuwatibu vijana walioathirika na dawa hizo.

"Bila vijana madhubuti wenye siha na afya njema, akili timamu na walioelimika, mipango ya kufikia ajira 300,000 haitafanikiwa," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana, alisema dawa za kulevya ni janga la kimataifa na Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizoathiriwa na tatizo hilo.

Alisema Zanzibar inakisiwa kuwa na takribani ya watu 10,000 wanaotumia dawa za kulevya na matumizi ya dawa hizo yanachochea maradhi mbalimbali yakiwamo saratani, magonjwa ya akili, maambukizi ya Ukimwi, homa ya ini na maradhi mengine ya kujamiiana.

# Mapato bandari Zanzibar yaongezeka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAPATO katika Shirika la Bandari Zanzibar yameongezeka kwa mwezi machi, mwaka huu hadi kufikia Sh. Bilioni 3.6 pamoja na faida ya Sh. bilioni 2.2.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar, Nahaat Mohamed Mahfoudh, alisema juzi wakati uongozi wa shirika hilo ulipokutana na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, ofisini kwake Vuga.

Nahaat alisema mafanikio hayo ni ya muda mfupi tangu kuanza kuboreshwa kwa huduma katika bandari huku akisisitiza kuwa mafanikio hayo yamepatikana licha ya changamoto ya janga la corona duniani pamoja na mfumuko wa bei.

Kutokana na mafanikio hayo Makamu wa Pili wa Rais alielezea kufurahishwa na kueleza kwamba serikali haitegemei kuona mabaya yoyote yanajitokeza katika eneo hilo kwa kuwa wameonyesha uwezo mzuri wa kazi zao.

Pia aliwasihi kuwa bandari ni eneo linalotoa huduma kwa jamii, hivyo ni vyema watendaji wake kuwa na utayari na ufanisi katika majukumu yao na hatimaye kufikia malengo na azma ya serikali.

Naye Waziri wa Miundombinu, Mawasiliano na Usafirishaji, Rahma Kassim Ali, alisema wizara kwa kushirikiana na shirika hilo, wamejitahidi kutatua changamoto zinazowakabili na nyingi wanazitatua kwa hatua ya awali ingawa ziko zinazowapa vikwazo na watazifikisha sehemu husika kwa ajili ya maelekezo zaidi.

Katika hatua nyingine, Hemed aliwataka watendaji wa serikali katika sekta mbalimbali kuwajibika ipasavyo hasa katika kusimamia makusanyo ya fedha katika maeneo yao ili kuchochea kasi miradi ya maendeleo.

Hemed alisema ni wajibu kwa watumishi kuhakikisha mapato yanaongezeka, ili serikali kuongeza kasi ya kuleta maendeleo kwa maslahi ya wananchi.

Alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, wakati akiomba ridhaa kwa Wazanzibari, alikutana na makundi mbalimbali na kuahidi mengi, hivyo ni vyema kwa watendaji kuongeza kasi zaidi kwa vile wao ndio watekelezaji wa yale aliyoyaahidi Rais.

Hemed aliwataka viongozi hao kuendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika maeneo yao ya kazi na zile wasizoziweza ni vyema wakaziwasilisha katika mamlaka za juu ili kuzifikisha sehemu husika.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Salum Khamis Rashid (kulia), alipofanya ziara katika ofisi hizo, Maruhubi, jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kesi 160 udhalilishaji zafunguliwa mwezi mmoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TANGU kuazishwa kwa Mahakama Maalum ya kushughulikia Kesi za Udhalilishaji Zanzibar, kesi 160 zimeripotiwa mahakamani hapo ndani ya mwezi mmoja kutoka Febuari 8 hadi Machi 8, mwaka huu, Unguja na Pemba.

Hayo yalielezwa jana na Mrajis wa Mahakama Kuu Zanzibar, Muhammed Ali Muhammed, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Vuga mjini Zanzibar.

Alisema kuazishwa kwa mahakama hiyo kumetokana na agizo la Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, baada ya uwapo wa matukio mengi ya kesi za udhalilishaji.

Muhammed alisema katika kesi hizo, mbili zimeshapatiwa hukumu na 158 zinaendelea kusikilizwa na kwamba kuanzishwa kwa mahakama hiyo huenda kukawa mwarubaini wa kutokomeza vitendo hivyo.

"Tokea kuanzishwa mahakama maalum ya kesi za udhalilishaji Febuari 8, mwaka huu, hadi Machi 8 kesi 158 zimefunguliwa. Kesi 94 zimefunguliwa mahakama maalum iliyoko Vuga mjini Zanzibar, Kesi 26 Kaskazini Unguja, Mahamonda, 21 Kusini Unguja Mwera, tisa Kusini Pemba Chakechake na 10 Wete Kaskazini Pemba na kesi mbili zimepatiwa uamuzi.

Akizungumzia changamoto kwa mahakama hizo alisema pamoja na mambo mengine, zinakabiliwa na uhaba wa mahakimu katika kushughulikia kesi hizo lakini serikali imeshatoa kibali cha kuajiri mahakimu wapya ili kusaidia katika ufanyaji kazi katika mahakama hiyo.

"Wakati wote kuanzia sasa tutapata mahakimu na kazi yao itakua kushughulikia kesi za udhalilishaji pekee. Hawatahusika na kesi za wizi wa kuku wala matunda," alisema.

Alisema kuwa kwa sasa kuna mahakimu wasiopungua 15 wanaoshughulikia kesi hizo katika mahakama za Unguja na Pemba.

Alisema bado kesi za udhalilishaji zipo nyingi ambazo zinazisikilizwa ikiwamo zilizoripotiwa kabla ya kuanzishwa kwa mahakama maalum hivyo bila ya uwepo wa jopo kubwa la mahakimu zitashindwa kusikilizwa kwa haraka.

Mrajis alisema katika usikilizaji wa kesi hizo zisichukue zaidi ya siku 90 na ziwe zimeshapatiwa uamuzi, hivyo kuongezeka kwa idadi ya mahakimu kutarahisisha utendaji na utoaji wa hukumu.

Alisema changamoto nyingine ni uhaba wa majengo kwa kuwa kwa sasa wanatumia majengo ya mahakama kwa kila mkoa Unguja na Pemba.

Naye Mkuu wa Utafiti na Ushauri katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Ramadhan Abdalla Nassib, alisema wamejipanga katika uendeshaji wa kesi za udhalilishaji katika mahakama maalum ikiwamo kutoa mafunzo kwa wanasheria na kuongeza uajiri kwa wanasheria wapya ambao watashughulikia kesi hizo.

Pia alisema mambo ya udhalilishaji yanahitaji stara, hivyo yapatikane majengo ya mahakama hizo kulingana na makosa yenyewe ili watu wawe huru kutoa ushahidi bila kudhalilishwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO 106/2021**

Ombi la **ABDULAZIZI NASIBU MTAKAHELA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **NASIBU RAMADHANI MTAKAHELA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **27/05/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 14/04/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**AGUSTINO FAUSTINI HHANDO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya KINGLION yenye namba ya usajili MC 318 CLR.Chassis No.LZL15P903KHL52683, Engine No.KLI62FMJ101152683.Y eyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: KRT/R-**B/520/2021**.

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

AGUSTINO FAUSTINI HHANDO anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SIMORAY yenye namba ya usajili MC 595 CBJ Chassis No.LD3PCK6J7J2006221, Engine No.SR162FMJ18106221.Y eyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: KRT/R-B/520/2021.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.13 OF 2021**
**In the matter of the Estate of the late GIBSON GEORGE MPILIMI of Miyuji Ward within Dodoma City Council**

**AND**
**In the matter of an application for letters Administration by HILDA SAMSON MPILIMI**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners
Objections to the grant should be filed on or before the **14 Day of May 2021.**
Dated at Dodoma this 20 day of April 2021

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.119/2021**

Ombi la **GLADNESS AINEA USIRI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **ISACK LAZARO MISEA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **18/05/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 21/04/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

*RICHARD PENNINGTON LYAMUYA,*
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki Yenye namba za usajili **MC 626BXT** .
Injini namba **AF7AJ1509821** na Chassis namba **MD625AF76J1A09748**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taafifa :
**MOSHI/TR/RB/774/2021**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MBEYA**
**SHAURI NO. 57/2021**
**ERASTO M.PERA..................MDA I**
**DHIDI YA**
**ACCESS BANK TANZANIA LIMITED......................WADAIWA**
**JEREMIA PERA........................**
**KWA :**
**JEREMIA PERA,**
**KUITWA SHAURIN**

Fahamu kwamba Erasto M.Pera amefungua Shauri dhidiyakokatika Baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa Tarehe 28.04.2021 saa2.30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya saiku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika Masijala ya Baraza la Aardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka Usipo hudhuria siku hiyo, Baraza litatoa Amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza Shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 31/03/2021.
**T.Munzerere**
**Mwenyekiti**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo MAKOLE**
**Usimamizi wa mirathi No.38/2021**
**Ombi la REBIDA ERENEST MWEMBE kuteuliwa**
**Msimamizi wa mirathi Marehemu BEZAREL MSUBA MASAU**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **30/4/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 21/4/2021**

## LOSS OF CERTIFICATE OF INCENTIVE

**TAKE NOTICE** that the above Certificate of Incentive issued by Tanzania Investment Center to **TRANSPAPER (T) LTD** is said to be lost. Whoever find it please report to the nearest Police station. Police Report **No. DAR/CHA/R-B/197157/2021**

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**ADAM LOTOOMONWOKI KILEVO**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI
**T 464 ATH - HONDA 250**
TAARIFA HII IMERIPOTIWA KITUO CHA POLISI TAREHE 13, APRIL 2021.
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI
**ARU/ARU/RB/202034/2021.**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

**Cornellius Mpina** mkazi wa Manispaa ya Shinyanga. Anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 421 **Kitalu "V"** eneo la Ngokolo Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Cornellius Mpina kwa simu namba **0623708128.** Rb namba **Shy/Rb/ 2021,** Control Namba **9910823396744.**

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## Baraza la Biashara kufanyiwa maboresho

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, ameahidi kufanya mabadiliko kwenye Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) sambamba na kuongeza ufanisi katika kuimarisha mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao chake na menejimenti na wafanyakazi wa TNBC juzi, Mwambe alisema baraza kama taasisi ni kiungo muhimu kati ya sekta za umma na binafsi na hivyo kuimarika kwake kutaleta matokeo chanya ikiwamo kukua kwa biashara na kuongezeka kwa uwekezaji.

"Kuongezeka kwa ufanisi wa baraza kutaliongezea na kutoa mchango stahiki wa kuziunganisha sekta za umma na binafsi kufanya majadiliano ya namna bora ya kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara, kuvutia uwekezaji na kuongeza mapato ya serikali," alisema Waziri Mwambe.

Waziri Mwambe aliyefanya ziara yake ya kwanza tangu ateuliwe kushika nafasi hiyo hivi karibuni, alisema ili taifa lisonge mbele kiuchumi lazima kuwe na sekta binafsi madhubuti na ambayo itakuwa jumuishi.

Amesema licha ya uchanga wa wizara, yeye na timu yake watahakikisha wanashirikiana na wadau wote katika sekta za uwekezaji, biashara na taasisi zote zilizopo kwenye wizara hiyo kuweka mikakati ya namna bora ya kuvutia zaidi uwekezaji na biashara.

"Mimi na timu yangu tumekuja kuona namna TNBC wanavyofanya kazi, kusikiliza changamoto zao pamoja na kupokea mawazo. Tunakusudia kuzileta pamoja sekta ya umma na binafsi kwa kuondoa changamoto na kuongeza ufanisi," alisema.

Waziri Mwambe mbali ya kuipongeza TNBC, alisema lina nafasi kubwa ya kuhakikisha sekta za umma na binafsi zinafanya kazi kwa karibu zaidi na kuongeza wigo wa uwekezaji na kuchochea ongezeko la ajira kwa vijana na pia kuongeza mapato ya serikali.

Waziri Mwambe aliahidi pia kufanya mazungumzo na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) hivi karibuni kuona namna bora ya ushiriki wake katika TNBC ili kupiga hatua mbele ya maendeleo ya taifa.

Aidha, Waziri alizitaka taasisi zote za umma kuachana urasimu, rushwa na kuwa rafiki kwa wawekezaji ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya ukuaji wa uchumi unaokadiriwa kukua kwa asilimia nane kwa mwaka.

Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alimhakikishia waziri na timu yake kuwa baraza litatoa ushirikiano mkubwa ikiwamo kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuwavutia uwekezaji.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Mohamed Mtesa, akipanga sehemu ya mashuka 200 na vitanda viwili vilivyotolewa na Mbunge wa Liwale, Zuberi Kuchauka juzi, kwa ajili ya hospitali ya wilaya hiyo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# TEF yataka marekebisho Sheria Huduma za Habari

**Na Christina Mwakangale**

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Deodatus Balile, amesema ipo haja ya serikali, vyombo vya habari na wadau wake, kukaa meza moja kufanyia marekebisho baadhi ya vifungu vilivyopo katika Sheria ya Huduma ya Habari ya Mwaka 2016.

Amesema sheria hiyo ina vifungu ambavyo vinatoa adhabu ya aina tofauti ikiwamo kufungia, kufutia usajili bila kutaja aina ya kosa.

Balile aliyasema hayo katika mahojiano na moja ya kipindi katika televisheni nchini, na kwamba inapotajwa chombo au mwandishi uandika habari ya kichochezi, kashfa bila kufafanuliwa adhabu ya makosa hayo, kunasababisha adhabu kuwakumba wasiohusika.

"Sheria ya kufungia vyombo vya habari iainishe aina ya kosa na adhabu. Mfano mwandishi mmoja wa chombo cha habari kilichoajiri waandishi zaidi ya 50, akifanya kosa adhabu ya kulifungia gazeti lote si sawa.

"Au pengine habari iliyotoka ukurasa wa tatu, ikatajwa ni ya kashfa na adhabu ikatolewa na mamlaka kwamba gazeti lote lifungiwe lenye kurasa zaidi ya 20, kutokana na kosa la ukurasa mmoja si sawa," alisema Balile.

Alisema, ifike wakati tasnia ya habari iwe na mamlaka za kudhibiti nidhamu, kusimia weledi zilizo huru ili kushughulikia makosa yatokanayo kitaaluma.

"Kuna makosa ya kitaaluma ambayo si kwamba yanakubalika ila hutokea. Kwa mfano miaka ya nyuma kuna mgonjwa aliyetakiwa kufanyiwa upasuaji wa mguu akapasuliwa kichwa, na aliyehitajika kufanyiwa upasuaji wa kichwa akafanyiwa ya mguu. Madktari kupitia baraza lao walishughulikia hili.

"Hata sisi waandishi wa habari iwe hivyo. Isiwe tu mkurugenzi wa halmashauri, mkuu wilaya, mkoa au meneja fulani anatoa tu amri ya kutoa amri kuwawka chini ya ulinzi waandishi wakati kuna msimamizi wa taaluma Baraza la Habari Tanzania (MCT), aachiwe kazi hii," alisema Balile.

Kadhalika, Balile alisema sheria iliyopo ambayo ilirithiwa kutoka mkoloni hadi iliyokuwa Sheria ya Magazeti ya Mwaka 1976 na sasa Sheria ya Huduma ya Habari ya mwaka 2016, viainishwe vipengele, aina ya kosa, adhabu pamoja na faini ili kuondoa mkanganyiko.

"TEF moja ya majukumu yetu ni kuboresha weledi wa habari. Baada ya kauli ya rais kwamba 'media' zifunguliwe,baadhi tu vilifunguliwa. Sasa ni wakati wa kushirikiana na serikali kurekebisha sheria. Ili ikisemwa hivi tafsiri iwe moja.

"Mfano inapotajwa hili ni kosa la uchochezi ibainishwe uchochezi nini maana yake, tujadili kwa pamoja ili kosa lisijirudie.


Katika Sheria ya Habari ya Mwaka 2016, Sura ya nne ya sheria hiyo inataja kuundwa kwa Baraza Huru la Habari, ijapokuwa awali wanahabari waliunda baraza hilo, likijulikana MCT, lililosajiliwa kama asasi ya kiraia.

Pia sheria hiyo, kuhusu mwandishi au chombo kutumbukia kwenye jinai aidha kutatokana na kashfa au masuala ya uchochezi na inatamka kuwa, mwandishi anaweza kuwa na hatia kama ataandika taarifa za kashfa kuhusu marehemu.



HABARI MICHEZO

# Arsenal yawashiwa taa ya kijani kwa Ryan




**LONDON,** England

ARSENAL ipo kwenye hatua nzuri ya mazungumzo ya kumsajili golikipa wa Brighton, Mat Ryan kwa mkataba wa kudumu, kwa mujibu wa Football Insider.

Golikipa huyo raia wa Australia alijiunga na 'Washikabunduki' hao Januari mwaka huu kwa mkopo, na tangu ametua klabuni hapo amekuwa akimfurahisha kocha Mikel Arteta ambaye anajaribu kuhakikisha anabaki hapo.

Kwa mujibu wa ripoti, klabu hizo mbili zinaendelea vema na mazungumzo na zinakaribia kufikia tamati hivi karibuni na kukubaliana bei ambayo inatarajiwa kuwa chini ya pauni milioni 10 ambayo iliainishwa awali na Brighton.

Kwa upande wa Brighton, Robert Sanches, amejiweka katika nafasi bora kama golikipa namba moja, hivyo kocha mkuu Graham Potter yupo tayari kumuachia Ryan kwenda Arsenal.

Ryan amecheza mechi 58 za timu ya Taifa ya Australia, na aliungana na Brighton akitokea Valencia mwaka 2017.

Amecheza jumla ya mechi 120 za Brighton, msimu huu akiwa akicheza 11 na ana jumla ya hati safi 27 kwenye Ligi Kuu England.

# Fernandez: Namkubali sana Pogba dimbani




**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Bruno Fernandes, ameeleza kwamba, anamkubali kiungo mwenzake wa timu hiyo, Paul Pogba.

Katika mahojiano na televisheni ya ManTV, Bruno alieleza namna ambavyo wamejuana na Pogba tangu alivyokuwa Juventus na kiwango kikubwa ambacho wawili hao wanacheza kwa kushirikiana uwanjani.

Bruno alieleza namna ambavyo mabeki na wachezaji wa timu pinzani wanavyopata wakati mgumu kipindi wanapokutana na wachezaji wawili wanaoweza kucheza na mpira ipasavyo.


Pogba alionekana kupoteza furaha yake katika timu ya Man United hivi karibuni, lakini hivi sasa ameonekana kupenda kusakata kabumbu akiwa na 'Mashetani Wekundu' hao.

"Nahisi Paul ni miongoni mwa wachezaji bora duniani hivi sasa, na huwa anatoa ushauri kwa wenzake kwenye vyumba vya kubadilishia nguo. Ni mcheshi sana," alisema Fernandes.

"Kwangu mimi, kucheza na Paul kunanifanya nionyeshe uwezo mkubwa. Kucheza na mtu anayejua kunanifanya nifanye mazuri zaidi na nahisi hilo limenifanya kuonyesha uwezo mkubwa sana tunapokuwa uwanjani."

Fernandez amekuwa ni mchezaji tegemeo wa Man United tangu asajiliwe klabuni hapo, akiwa amecheza mechi 32 za Ligi Kuu na kufunga mabao 16, huku akitoa pasi za mwisho 11.

# United yaachana rasmi na Woodward



**MANCHESTER,** England

BAADA ya Manchester United kujitoa kwenye mashindano mapya ya Ulaya (European Super League), klabu hiyo imetangaza rasmi kuwa Mkurugenzi wake Mkuu, Ed Woodward, atajiuzulu nafasi hiyo mwishoni mwa msimu huu wa 2021.

Woodward alijiunga na Man United mwaka 2005 na kuisaidia timu hiyo katika nyakati mbalimbali kabla ya kuchukua nafasi ya David Gill kama mkurugenzi mkuu mwaka 2013.

Man United chini ya Woodward imekuwa ikikosolewa kwa kushindwa kubeba taji la Ligi Kuu England sambamba na kutokuwa na sera nzuri ya usajili kwenye klabu hiyo.

Wadau na mashabiki wengi wa United wamekuwa wakishinikiza Woodward kuondolewa klabuni hapo kwa muda mrefu na pengine hii ikawa ni habari njema kwa wengi waliokuwa hawamuhitaji tena kiongozi huyo.

"Ninajisikia fahari kuitumikia United, ni heshima kubwa kuitumikia moja ya klabu kubwa duniani kwa takribani miaka 16," alisema Woodward akinukuliwa na BT Sport.

"Klabu ipo katika muelekeo mzuri wa baadaye na utakuwa ni wakati mgumu kuondoka mwishoni mwa mwaka huu.

Naye mmiliki wa Man United, Joel Glazer, alisema ulikuwa wakati mzuri kufanya kazi na Woodward na amewaacha vizuri.

"Kwa niaba ya kila mmoja, Manchester United, ninamshukuru sana (Ed Woodward) kwa utendaji kazi wake na kujituma bila kuchoka," alisema Glazer.

"Mchango wake kwenye klabu ni mkubwa na ataendelea kukaribishwa Old Trafford kama mwanafamilia wa Manchester United."

## HABARI MICHEZO




# Ronaldo basi tena kutua Real Madrid

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Klabu ya Real Madrid, Florentino Perez, amesema Cristiano Ronaldo hatorejea hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Perez ambaye anajulikana kwa mtindo wake wa usajili wa 'Galactico' (wachezaji wakubwa), amechaguliwa tena kubaki kwenye uongozi wa miamba hiyo ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Awali iliripotiwa kwamba, Madrid inafanya juhudi za kutaka kumsajili Ronaldo ambaye ni mshindi mara tano wa Ballon d'Or, baada ya kuondoka Real na kutua Juventus akiwa mfungaji bora wa klabu mwaka 2018, lakini hakuna dili linalopangwa kurejeshwa kwa Mreno huyo mwenye umri wa miaka 36.

Perez aliiambia El Chiringuito: "Christiano Ronaldo hatokuja tena Real Madrid.

"Haileti maana yoyote, ana mkataba na Juventus. Nampenda sana ametupa vitu vingi."

"Hatujafanya mazungumzo yoyote naye wala Juventus, na kwa uhakika kabisa hakuna mpango wa kumrejesha hapa Ronaldo, yeye ni mchezaji wa Juventus kwa sasa na ana mkataba kule."

## Solskjaer: Man inaweza kutwaa ubingwa EPL




**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema mambo ya kushangaza huwa yanatokea kwenye soka, hivyo anaweza kuipiku Manchester City na kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Man United imepitwa pointi sita na Man City ambao wanaongoza msimamo wa Ligi hiyo wakiwa na nafasi kubwa ya kubeba taji hilo.

Ushindi ambao Man United iliupata msimu huu dhidi ya Man City na kipigo ambacho timu hiyo ilipokea kutoka kwa Leeds United imekuwa moja kati ya mambo yanayoashiria kwamba huenda upepo ukabadilika.

"Kila mechi ni muhimu kwa Manchester United na hatutakubali kuachia pointi kwenye mechi zetu zijazo, unaniuliza kama tunaweza kuipata Man City?

"Mambo ya ajabu huwa yanatokea kwenye soka, yule anayeongoza anaweza kuanguka, ni kweli wana kikosi imara na wana matumaini makubwa ya kupata taji," alisema akinukuliwa na BT Sport.

"Ninachokiamini ni kufanya kazi yetu kwa ufasaha ikiwa ni pamoja na kushinda kila mechi ya ligi iliyo mbele yetu na baada ya hapo ndio tutawaangalia wao kama watapoteza au la.

"Hatuwezi kukibadili kile wanachofanya, tunatakiwa kucheza mechi zetu na kuzingatia tuna mechi ngumu nyingi mbele yetu."

# Mourinho asaka kibarua Celtic

**LONDON,** England

BAADA ya kufungashiwa virago pale Tottenham Hotspur Jumatatu, inadaiwa kuwa Kocha Jose Mourinho, amejitosa katika kinyang'anyiro cha kuinoa timu ya Celtic ya nchini Scotland.

Hata hivyo, timu ya Valencia nayo inahusishwa na kocha huyo raia wa Ureno huku mmiliki wa klabu hiyo, Peter Lim akijiandaa kumtimua kocha wa sasa, Javi Gracia, ambaye amekaa na timu hiyo kwa miezi 17 pekee.

Mourinho alifungashiwa virago Jumatatu wiki hii baada ya kupoteza matumaini ya klabu hiyo kumaliza katika nne baada ya sare ya 2-2 dhidi ya Everton.

Kocha huyo wa zamani wa Porto, Chelsea, Inter Milan, Real Madrid na Manchester United, alijiunga na Spurs Novemba 2019 akichukua nafasi ya Mauricio Pochettino.

Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy, amesema hofu yake kubwa ilikuwa ni kupoteza wachezaji wake 10 ambao wangeondoka klabuni hapo msimu huu wa majira ya joto kama hasingemfuta kazi Mourinho.

Levy alikuwa na wasiwasi zaidi kuhusu Muingereza Harry Kane na Dele Alli, 25, pamoja na mshambuliaji wa raia wa Wales, Gareth Bale, 31, ambaye alijiunga na klabu hiyo kwa mkopo kutoka Real Madrid



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLABU ZOTE ENGLAND ZAJITOA SUPER LEAGUE

## Zawaomba radhi mashabiki Rais wa UEFA apokea uamuzi huo kwa furaha, yasema...

**LONDON,** England

KLABU zote sita za Ligi Kuu England, zilizojihusisha na ligi mpya Ulaya, (European Super League), zimejiondoa rasmi katika mashindano hayo, kwa mujibu wa BBC Sport.

Manchester City ilikuwa ya kwanza kujiondoa baada ya Chelsea kuashiria nia ya kuandaa waraka wa kujiondoa. Klabu nyingine nne, Arsenal, Liverpool, Manchester United na Tottenham pia zimefuata mkondo huo.

Man City imethibitisha kwamba "wamefanya rasmi mchakato wa kujiondoa" katika ligi hiyo, huku Liverpool ikisema kujihusisha kwao katika ligi hiyo iliyopendekeza kujitenga "kumesitishwa".

Man United walisema baada ya "kutathmini hisia za mashabiki wetu, serikali ya Uingereza na wadau wengine" wameamua kutoshiriki.

Arsenal waliomba radhi katika barua ya wazi kwa mashabiki wao na kusema kwamba "walifanya makosa", na kuongeza kuwa wanajiondoa baada ya kuwasikiliza wao na "jamii kubwa ya soka".

Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy, amesema klabu hiyo inasikitishwa na "wasiwasi na ghadhabu" iliyosababishwa na pendekezo hilo.

**Chelsea wamethibitisha kwamba "wameanza mchakato rasmi wa kujiondoa katika kundi hilo" walilojiunga nalo "mwishoni mwa wiki iliyopita".**

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya (UEFA), Aleksander Ceferin (pichani), amekaribisha hatua hiyo, na kusema: "Sasa wamerudi kwenye mkondo na ninajua kwamba wana mengi ya kufanya si tu kwa washindani wetu bali pia kwa michezo yote ya Ulaya.

"Cha msingi kwa sasa ni kusonga mbele, kuimarisha tena umoja ulioletwa na mchezo huu awali na siku zijazo."

Klabu hizo 'sita kubwa' za soka nchini Uingereza zilikuwa sehemu ya mashindano hayo, ambayo yanajumuisha Atletico Madrid, Barcelona na Real Madrid za Hispania pamoja na AC Milan, Inter Milan na Juventus za Italia, zilizotangaza mpango wa kuanzisha ligi nyingine, ambayo ingebuni mashindano ya katikati ya wiki.

Ililaaniwa vikali na mashabiki, mamlaka za soka na mawaziri wa serikali nchini Uingereza na Ulaya ikiwamo Uefa na vyama vya ligi.

Karibu mashabiki 1,000 walikusanyika nje ya Uwanja wa Chelsea wa Stamford Bridge kabla ya mchezo wao dhidi ya Brighton siku ya Jumanne kupinga kujihusisha kwa klabu yao.

Hakuna upande wowote wa Hispania na Italia ambao umetoa taarifa baada ya timu sita za Ligi Kuu kujiondoa.

## KWA UFUPI

### MOURINHO ATAKA KAZI CELTIC
JOSE Mourinho, ambaye alifukuzwa kazi kule Tottenham Hotspur Jumatatu, amejitosa katika kinyang'anyiro cha kuwania kuwa kocha wa Celtic. **(Sun)**

### MBAPPE HUYO MADRID
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, ameanza mkakati wa kuhamia Real Madrid. Mshambuliaji huyo wa Ufaransa bado hajakubali kutia saini ya mkataba mpya kule PSG na kwa muda mrefu amehusishwa na tetesi za kuhamia Madrid. **(Goal)**

### RODGERS AIKATAA SPURS
KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers mwenye umri wa miaka 48, amepuuzia mbali tetesi zinazomhusisha na uhamisho wa kwenda Tottenham Hotspur. **(Talksport)**

### AGUERO APEWA MIAKA MITATU
BARCELONA wamempa ofa ya mkataba wa miaka miwili mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32. Raia huyo wa Argentina yuko huru kuondoka kwa uhamisho wa bure mkataba wake utakapomalizika pale Etihad mwishoni mwa msimu huu. **(TyC Sports)**

### VALENCIA YAMUWANIA MOURINHO
KLABU ya Valencia pia imehusishwa na Jose Mourinho, wakati mmiliki wa klabu hiyo, Peter Lim anajiandaa kumtimua kocha wa sasa, Javi Gracia. **(Todofichajes)**

### BAILLY KUTUA BETIS
REAL Betis wanataka kumsajili mlinzi wa Ivory Coast, Eric Bailly, mwenye umri wa miaka 27, kutoka Manchester United mwishoni mwa msimu huu. **(Sun)**

### VILLA WAJITOSA KWA LINGARD
ASTON Villa huenda wakamnunua kiungo wa kati wa Manchester United na England, Jesse Lingard mwishoni mwa msimu huu. West Ham United pia wanapania kumpatia mkataba wa kudumu Lingard mwenye umri wa miaka 28, ambaye amekuwa akiwachezea kwa mkopo tangu Januari. **(Football Insider)**

### CALETA-CAR AJIPELEKA LIVER
MLINZI wa Marseille na Croatia, Duje Caleta-Car mwenye umri wa miaka 24, ana matumaini Liverpool itafufua azma ya kumtaka ajiunge nao hasa wakati huu ambapo klabu yake iko tayari kumwachilia. **(RMC Sport, via Team Talk)**

### JOHNSTONE KUBAKI BROMWICH
KLABU ya West Bromwich Albion wameamua kubaki na golikipa wao, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 28. Manchester United na West Ham zilikuwa zinamtolea macho nyota huyo wa England. **(Express and Star)**

### TAVARES AWANIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE United wanamtaka beki wa Benfica chini ya umri wa miaka 21 raia wa Ureno, Nuno Tavares. (Record, via Sport **Witness)**

### LEVY ALIMHOFIA MOURINHO
MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy, anahofia huenda hadi wachezaji 10 wangeondoka klabuni hapo msimu wa majira ya joto, kama asingelimfuta kazi Jose Mourinho. **(Eurosport)**

# HABARI MICHEZO

## NCHIMBI AFUNGUKA KUFUNGA YANGA BAADA YA MIEZI 14

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya straika wa Yanga, Ditram Nchimbi, kusema kwamba hakumbuki mara ya mwisho kufunga bao ilikuwa lini, takwimu zinaonyesha imemchukua mwaka mmoja na miezi miwili [miezi 14] ya ukame wa kucheka na nyavu kabla ya juzi kulifumania lango la Gwambina FC wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-1.

Juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Nchimbi alifunga bao kwenye dakika ya 19, akiisaidia timu yake kushinda 3-1 dhidi ya Gwambina kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara na kuifanya izidi kupaa kileleni kwa kufikisha pointi 57.

"Nimefurahi nimefunga. Nilisema siku chache nyuma kuwa nitafunga na kweli leo nimetimiza ahadi, unajua siyo kwenye mpira, hata kwenye maisha kuna changamoto nyingi na watu watakusema sana, lakini unapaswa kuchukulia kama changamoto na kuifanyia kazi. Ndiyo maana mimi pamoja na watu kunisema sana, lakini sikuhamanika. Niliendelea na mazoezi nikajua ipo siku nitafunga tu na kweli leo nimefunga, maisha yanaendelea," alisema Nchimbi.

Mara ya mwisho kwa mchezaji huyo kufunga bao ilikuwa ni Februari 29, mwaka jana, alipopachika mabao mawili, Yanga ikiichapa Alliance FC mabao 2-0 msimu uliopita. Lakini alivyoulizwa kwamba mara yake ya mwisho kucheka na nyavu ilikuwa lini, Nchimbi alisema: "Sikumbuki ilikuwa lini nimefunga ila nimefurahi kuona kwamba nimefunga kwa kuwa ushindi ni jambo la msingi na tumefurahi".

Hilo linakuwa ni bao la kwanza la Nchimbi msimu huu, ambaye pia anaichezea timu ya taifa, Taifa Stars.

Msimu uliopita, Nchimbi alimaliza ligi akiwa na mabao sita, matatu aliyafunga akiwa na Polisi Tanzania na matatu akiwa Yanga.

Yanga ilimsajili mchezaji huyo kwenye kipindi cha dirisha dogo akitokea Polisi Tanzania Ligi Kuu msimu uliopita wa 2019/20 na hii ni baada ya kuifunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mechi ya Ligi Kuu.

Nchimbi wakati huo akiichezea Polisi Tanzania, alifunga mabao hayo dhidi ya Yanga na timu hizo zikatoka sare ya mabao 3-3 na hapo ndipo taratibu za usajili zilipofanyika. Wakati huo Nchimbi alikuwa akiichezea Polisi Tanzania kwa mkopo akitokea Azam FC.

### NILIKWAMBIA LAKINI...



Wachezaji wa Yanga wakishangilia kwa staili yao mpya, kwa kiungo wa timu hiyo, Mukoko Tonombe, kuonekana kama anatoa darasa kwa Ditram Nchimbi (Kulia aliyepiga magoti), baada ya kufunga bao la kwanza wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Gwambina FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. Hilo ni bao la kwanza kwa Nchimbi kufunga katika kipindi cha miezi 14. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mgosi atoa neno mtifuano Ligi ya Wanawake ikirejea

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu ya wanawake Tanzania Bara inatarajiwa kuendeleo kesho, Ijumaa kwa kupigwa michezo mitatu ambapo JKT Queens itaikaribisha Kigoma Sisterz katika dimba na Maj.Gen Isamhuyo uliopo Boko, Dar es Salaam.

Michezo mingine itakayopigwa siku hiyo ni TSC Queens wakiwa nyumbani kuwakaribisha Mlandizi Queens kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza wakati Tanzanite SC itakuwa mwenyeji wa Mapinduzi Queens katika Uwanja wa Fountain Gate Arena.

Ligi hiyo itaendelea tena Jumamosi wiki hii kwa mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo, Simba Queens, kushuka ugenini katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza dhidi ya wenyeji wao, Alliance Girls.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema wamejipanga vizuri n kuhakikisha wanapata matokeo mazuri dhidi ya Alliance Girls.

"Malengo yetu msimu huu ni kuendelea kufanya vizuri na kutetea ubingwa wetu, nina imani tutafanikiwa kulingana na maandalizi tuliyofanya, tutacheza kwa nidhamu ya hali ya juu dhidi ya wapinzani wetu tutakaokutana nao," alisema Mgosi.

Siku hiyo pia Yanga Princess watakuwa na kibarua nyumbani katika Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam ikiwakaribisha Unyanyembe na mchezo mwingine utakuwa kati ya Baobab Queens na Ruvuma Queens utakaopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Timu hizo zimekamilisha michezo 15 ya mzunguko wa kwanza huku Simba ikiongoza msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 39 ikifuatiwa na Yanga yenye alama 38 na JKT Queens ikishika nafasi ya tatu pointi zake 36.

Alliance Girls inashika nafasi ya nne baada ya kujikusanyia pointi 28, Ruvuma Queens ikifuata kwa alama zake 25 na nafasi ya sita ikishikiliwa na Mlandizi Queens kwa pointi 23 wakiwa na pointi sawa na Baobab waliopo nafasi ya saba.

Nafasi ya nane ni Tanzanite SC kwa alama 19, TSC wakifuata na pointi zake 14, kisha Kigoma Sisterz yenye pointi 12, Mapinduzi Queens ikiwa nafasi ya 11 kwa alama tatu na ES Unyanyembe ndiyo inayoburuza mkia ikiwa nafasi ya 12 kwa kutokuwa na pointi yoyote hadi sasa kwenye michezo yote 15 iliyocheza.

## SMZ waanza kujifua michuano ya Majeshi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU za Kanda za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), zinaendelea na mazoezi makali kuelekea michuano ya Majeshi (BAMATA) inayotarajiwa kufanyika Juni 5-16 mwaka huu mkoani Dodoma.

Michuano hiyo inatarajiwa kushirikisha Kanda nane za Majeshi ambazo ni Kanda ya Ngome, JWTZ Visiwani, JKT Uhamiaji, Polisi, Magereza, Zimamoto na SMZ.

Kanda ya SMZ ndio mabingwa watetezi wa jumla wa michuano hiyo kwa mwaka 2019 ambapo mwaka 2020 mashindano haya hayakufanyika kutokana na janga la Corona.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kanda ya SMZ, Sheha Mohmmed, alisema timu zote zinafanya mazoezi yake asubuhi katika kujiandaa na michuano hiyo ambayo inashirikisha kanda nane.

Alisema mchujo wa mwisho wa wachezaji kwa upande wa kanda yake, unatarajiwa kufanyika Mei 20, mwaka huu ili kupata wachezaji watakaoshiriki michuano hiyo.

Alisema kwa upande wa Kanda ya SMZ, imekusanya idara zake tano ambazo zinaunda kanda moja.

Alizitaja idara zinazounda Kanda ya SMZ kuwa ni Jeshi la Mafunzo, JKU, Zimamoto, KMKM na KVZ.

"Kanda yetu ni muungano wa idara zetu tano ambapo kila idara imetoa wachezaji kulingana na michezo inayofanyika, halafu tutakuwa na mchujo ili kupata wachezaji wazuri watakaoshiriki mashindano haya," alisema.

Michezo wanayotarajia kushiriki katika mashindano hayo ni soka kwa wanaume, mpira wa pete kwa wanawake, huku mpira wa kikapu, wavu, mikono, riadha na shabaha ikiwa ni kwa wote, wanawake na wanaume

Michezo
Alhamisi Aprili 22, 2021
Nipashe




HABARI UK.22

Klabu zote England zajitoa Super League

# SIMBA YAIKALIA YANGA KOONI MBIO UBINGWA

●●● Sasa kukamilisha hesabu kwa Gwambina FC baada ya kuichakaza viwili Kagera Sugar huku...

**Na Adam Fungamwango**

MKONGOMANI Chris Mugalu na raia wa Msumbiji, Luis Miquissone, jana walikuwa mashujaa wa Simba baada ya kila mmoja kucheka na nyavu wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar.

Ilikuwa ni mechi kali ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa katika Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Lakini pia ni matokeo ambayo wachezaji, benchi la ufundi, wanachama na mashabiki wa Simba, walikuwa wanayahitaji ili kupunguza pengo la pointi hasa baada ya watani zao wa jadi, Yanga, juzi kupata ushindi wa mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa dhidi ya Gwambina FC na kuzidi kujichimbia kileleni.

Dakika ya tano tu ya mchezo, Mugalu alianza kulitia msukosuko lango la Kagera Sugar alipopata pasi kutoka kwa Miquissone akiwa ndani ya eneo la hatari akiangalia golini kwake, lakini aligeuka ghafla na kupiga shuti lililotoka sentimeta chache langoni.

Mashabiki wa Simba walianza kupata furaha dakika ya 12, baada ya kupata bao lililofungwa na winga wao machachari, Miquissone kwa shuti kali la karibu, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Clatous Chama alipokokota mpira kwa umbali mrefu na kuingia nao ndani ya eneo la hatari, kabla ya kummegea pande mfungaji, ikiwa ni 'assist' (pasi ya mwisho)yake ya 12 msimu huu.

Mugalu alikosa tena bao, alipopaisha mpira juu, akiunganisha krosi ya Miquissone dakika ya 22, lakini alisawazisha makosa yake dakika moja baadaye alipopachika mpira wavuni, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Mzamiru Yassin aliyemmegea pasi Miquissone, naye akampasia Hassan Dilunga, ambaye alimdokolea mfungaji aliyepiga shuti la kuburuza lililomshinda kipa Ramadhani Chalamanda na kujaa wavuni.

Kipindi cha pili, Kagera Sugar inayofundishwa na kocha wa zamani wa Biashara United, Francis Baraza, ilibadilika na hasa baada ya kuingia kwa Hassan Mwatarema ambaye pamoja na kucheza soka safi, lakini pia alikuwa na matumizi makubwa ya nguvu kiasi cha kuonyeshwa kadi ya njano.

Ni kipindi ambacho lilishambuliwa lango la Simba, huku wageni wao wakishambulia kwa kushtukiza. Wachezaji Yusuph Mhilu, Nassor Kapama, Ally Nassor 'Ufudu', walipata nafasi lakini hawakuwa makini na mashuti yao ama yalitoka nje au kuishia mikononi mwa kipa bora kwa sasa, Aishi Manula.

Pamoja na mabadiliko ya kocha wa Simba, Didier Gomes ya kuwatoa, Hassan Dilunga, Mzamiru na Mugalu na nafasi zao kuchukuliwa na Rally Bwalya, Erasto Nyoni na Meddie Kagere, bado kipindi cha pili kilionekana kuwa kigumu kwa timu zote mbili.

Kwa matokeo hayo, Simba ambayo Jumamosi itashuka tena uwanjani ugenini dhidi Gwambina FC, bado inaendelea kukamata nafasi ya pili, ikiwa imefikisha pointi 55, mbili nyuma ya vinara wa Ligi Kuu, Yanga ambao wana pointi 57 mpaka sasa. Hata hivyo, Simba bado ina mechi tatu mkononi, kwani imecheza mechi ya 23, huku Yanga wakiwa wamecheza mechi 26.

HUNIWEZI...




Kiungo wa Kagera Sugar, Peter Mwalyanzi (Kushoto), akipata tabu kumzuia winga wa Simba, Luis Miquissone, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba jana na 'Wekundu wa Msimbazi' hao kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: SIMBA**

## Ntibazonkiza achafua hewa Yanga, atuliza

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mahiri wa Yanga, Saido Ntibazonkiza licha ya kuonekana 'kuchafua hewa' ndani ya klabu hiyo kutokana kitendo alichokifanya juzi, amewatuliza wanachama na mashabiki wa Yanga kwa kusema kuwa yaliyotokea uwanjani siku hiyo ni mambo ya kawaida na yamekwisha, kikubwa timu yake imepata ushindi na waangalie mbele.

Mchezaji huyo raia wa Burundi hakushangilia bao la tatu alilofunga, licha ya kwamba alifunga kwa umaridadi mkubwa, lakini pia aliomba kufanyiwa mabadiliko'sab' baada ya kufunga na licha ya Kocha Mkuu, Juma Mwambusi, kutoitika wito wake huo, alivua jezi na kutoka moja kwa moja uwanjani huku wachezaji wenzake na benchi la ufundi wakimsihi arejee lakini alikaidi na kuelekea kwenye vyumba vya kubadilishia.

"Tuko vizuri, mambo haya kuna wakati yanaweza kutokea, lakini ni pale pale tu kwenye mechi, ikiisha nalo limekwisha, na hii inatokea sehemu yoyote duniani kwenye maisha ya soka. Wachezaji hatuna tatizo, kutoshangilia mimi si tatizo, kikubwa ni ushindi tu," alisema.

Kwa bahati nzuri ni kwamba tukio hilo lilitokea kwenye dakika za majeruhi, kwani mwamuzi alipuliza kipenga cha kumaliza mechi hiyo, hata hivyo baada ya mechi kumalizika, ilionekana kabisa kuwa mambo hayakuwa sawa.

Alipoulizwa Juma Mwambusi alisema kuwa anadhani mchezaji huyo alizidiwa na furaha baada ya kufunga bao, ndiyo maana amefanya kitendo hicho.

Ni tukio ambalo kila mmoja, viongozi, wachezaji wenzake, wanachama na mashabiki wa Yanga kila mmoja amekuwa akiliongea, wengine wakidai anatoa ujumbe kuwa yeye si mchezaji wa kukaa benchi, wengine wakidai ni utovu wa nidhamu.

"Hana adabu, inamaana pale kwenye timu kuna wengine wa kukaa tu benchi na wengine wa kucheza kila siku, mnawapa thamani kubwa sana wachezaji wa kigeni, wanafika wanaleta dharau, wakati hawajaipa mafanikio timu. Ili iwe timu lazima tusajiliwe wengi, asipoomba msamaha katika mazoezi, aisee hatutakubali, wachezaji wapya hawajiheshimu tofauti na tuliocheza nao hapo nyuma," alisema mchezaji mmoja wa klabu hiyo ambaye aliomba hifadhi ya jina lake.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >